# Nipashe

Jumamosi Mei 11, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579915

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper





UKURASA 13



## Mganda alivyochangamkia fursa msiba wa Dk. Mengi

UKURASA 2




# Zitto, mawaziri wachuana vikali

**ATAKA** serikali ieleze Tril. 18/- zilivyotoa ajira, kukuza uchumi...*Endelea Uk. 2*



## MVUA KUBWA MFULULIZO ZAJA

UKURASA 3

Wananchi, waendesha pikipiki wakipita kwa shida kwenye maji ya mafuriko katika Barabara ya Morogoro, eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam kutokana na mvua kubwa iliyonyesha jana. Picha ndogo: Gari likipita kwa shida katika eneo hilo, huku wakazi wa Tandale kwa Mtogole wakitoa maji nje ya nyumba yao. **PICHA: JOHN BADI**

## Majaliwa awashauri wawekezaji kuhusu ajira

UKURASA 2

**MICHEZO** VIINGILIO KUIONA SEVILLA HADHARANI UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Majaliwa awashauri wawekezaji kuhusu ajira

Na Beatrice Moses

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewataka wawekezaji nchini kuboreshe mikataba ya ajira ili nao wafanyakazi wawe na uhakika na ajira zao.

Majaliwa aliyasema hayo juzi kwenye sherehe za kutimiza miaka 50 ya kampuni ya mafuta ya TOTAL nchini, zilizofanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, mabalozi, Rais wa TOTAL Africa, Stanislas Mittelman, makandarasi na wafanyabiashara na wateja bidhaa za kampuni hiyo.

"Mtoe kipaumbele cha ajira kwa Watanzania ili kuunga mkono jitihada za Serikali za kutengeneza mianya ya ajira kwa watanzania wa aina zote, ili wananchi waone maana ya uwekezaji wenu," alisema.

Waziri Mkuu alisema uwekezaji huo umewawezesha Watanzania zaidi ya 800 kunufaika na ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kutoka katika kampuni hiyo.

Alisema Serikali kwa upande wake imeendelea kutengeneza mazingira ya biashara na uwekezaji kwa kuboresha mifumo mbalimbali ya uwekezaji hapa nchini, kwa lengo la kuwezesha makampuni yote yaliyowekeza ikiwamo TOTAL kunufaika.

Alisema Serikali inafanya maboresho ya miundombinu ya uwekezaji ikiwamo reli, barabara, nishati, maji na viwanja vya ndege na hata ndege zenyewe ili kurahishisha usafirishaji wa bidhaa zinazozaliwa ziweze kutoka eneo moja na kupelekwa eneo lingine.

"Rais Dk John Magufuli kupitia Baraza la Biasahara mara kwa mara amekuwa anakutana na jumuiya ya wafanyabishara wa nchini kujadili na kupitia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazowakabili wafanyabiashara na kuwakwaza katika kufanya biashara," alisema.

Alisema wameanza utekelezaji wa mpango mkakati wa kuboresha mazingira ya uwekezaji wa biashara nchini, wanafanya mapitio ya vivutio

INAENDELEA UK. 4

# Zitto, mawaziri wachuana vikali

Na Sanula Athanas, DODOMA

MCHUANO mkali ulitokea bungeni jana wakati Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe (ACT-Wazalendo) alipohoji kuhusu kile alichodai kuporomoka kwa uchumi wa Tanzania licha ya serikali ya awamu ya tano kutumia Sh. trilioni 18.7 kuboresha miundombinu.

Hoja hiyo ya Zitto ilizua mchuano kati ya yake na mawaziri wenye dhamana ya fedha za mipango, Dk. Philip Mpango na naibu wake, Dk. Ashatu Kijaji, wakati wa mjadala wa hotuba ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka ujao wa fedha.

Katika hoja yake , Kiongozi huyo wa ACT-Wazalendo alisema katika kipindi cha miaka minne, Wizara ya Ujenzi imechukua asilimia 46 ya bajeti yote ya maendeleo, lakini haijatoa matokeo ya kuridhisha kwenye ukuaji wa uchumi.

"Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya fedha ambazo tumeziingiza kwenye wizara hii ni Sh. trilioni 18.7 sawa na asilimia 46 ya jumla ya fedha za bajeti ya maendeleo ya nchi ambayo ni Sh. trilioni 40.6.

"Kwa hiyo, asilimia 46 ya bajeti ya maendeleo unaishika wewe Kamwelwe na manaibu wako wawili. Wabunge wana haki ya kuuliza, kiasi hiki cha fedha ambacho tulichokiingiza kwenye wizara hiyo mpaka sasa kimezalisha viwanda vingapi?

"Tunazungumza kuhusu namna ambavyo fedha ambazo tunameingiza kwenye miradi kama reli, ndege, zinachocheaje sekta nyingine za uchumi?

"Tungepata maelezo ya serikali hapa, kwamba tumeingiza Sh. trilioni 18.7 na matokeo yake ni nini? Waziri Mpango analijua sana hili, kwamba moja ya sekta zinazopaswa kuonyesha zilivyochangia uchumi ni ujenzi.

"Kwanini sisi ambao tunaingiza fedha nyingi kiasi hiki, na bado kasi ya ukuaji wa uchumi iwe ni ndogo? Leo hii tunabishania makisio ambayo IMF wameyatoa ya asilimia nne na kadhalika.

"IMF na Waziri Mpango hawajakanusha makisio haya, wamekanusha 'leaked report' (ripoti iliyovuja) lakini makisio bado ni yale yale. Hata ukichukua makisio ya serikali ya asilimia sita, lakini 'before' (kabla) serikali ya awamu ya tano iingie madarakani 'economy' (uchumi) yetu ilikuwa inakua kwa asilimia 'for 10 years' (kwa miaka 10).

"Tangia serikali ya awamu ya tano imeingia madarakani, Sh. 18 trilioni zimeingizwa kwenye 'construction' (ujenzi) lakini 'sector growth rate' (kasi ya ukuaji wa kisekta) iko chini, kwa nini? Zitto alihoji.

Alitolea mfano nchi ya Kenya kwamba imejenga reli ya kisasa kwa mkopo mkubwa, lakini sekta yao ya ujenzi imekua kwa asimilia 1.5.

"Hata mkiacha ile asilimia nne ya IMF, twendeni na ile ya serikali ya asilimia sita, ni kwa sababu mipango yetu ya maendeleo ya miundombinu ni kutoa fedha kwenda nje na hatuingizi ndani na ndiyo maana mzunguko wa fedha ni mdogo sana, mmewapa kazi makandarasi wa nje, wanaagiza malighafi zote kutoka nje," Zitto alisema.

Aliongeza: "Mnakusanya kodi kwa muuza nyanya kumlipa Muturuki, naye anapeleka Uturuki ndiyo maana uchumi haukui, hata mjenge hoja namna gani, nimeona ile ya serikali kwenda IMF, kusema

INAENDELEA UK. 8



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akipokea zawadi ya sanamu la Twiga kutoka kwa Rais wa kampuni ya Total Afrika, anaeshughulika na masuala ya Masoko na Huduma, Stanislas Mittelman, katika hafla fupi ya kutimiza miaka 50 ya kampuni hiyo, iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mganda alivyochangamkia fursa msiba wa Dk. Mengi

Na Salome Kitomari

RAIA wa Uganda, Molakya Geofrey, juzi alichangamkia fursa ya biashara ya kuuza vifaa vya kuwekea funguo, baji za picha ya aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Marehemu Dk. Reginald Mengi.

Mganda huyo ambaye alionekana akiuza vitu hivyo kwa Sh. 1,000 kwa watu waliokuwa kwenye mistari ya kwenda kuaga mwili wa Dk. Mengi katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Moshi Mjini.

"Baada ya kusikia taarifa za kifo cha mpendwa wetu Dk. Mengi, niliingia kwenye Facebook na kubaini watu wengi wanampenda (Dk. Mengi) sana. Kama raia wa Uganda niliona ni fursa na kutengeneza vifaa vya kuwekea funguo na baji za kuvaa shingoni," alisema. Alisema upendo anaoweza kuuonyesha kwa Dk. Mengi ni kuchangamkia fursa ya kujipatia kipato kwa ajili ya maisha yake, na kwamba hivi karibuni atatengeneza kalenda atakazoziuza nchi mbalimbali.

"Nimeonyesha upendo wa hali ya juu kwa kuwa nimetoka Uganda nikapitia Kenya na sasa nipo Tanzania, nauza vitu hivi ambavyo vinanipatia kipato, nafanya utalii, lakini nafanya kitu cha upendo kwa mtu aliyependwa na Watanzania," alisema.

Alisema baada ya kuona mapokezi ya Mwenyekiti kuanzia Uwanja wa Ndege wa KImataifa wa Julius Nyerere (JNIA) na kutembezwa kwenye bararabara mbalimbali na baadaye siku ya kuaga na kupokelewa mkoani Kilimanjaro, aliona ni fursa kubwa na muhimu kwake.

Vifaa hivyo vilikuwa na picha mbalimbali za Dk. Mengi ikiwamo ambazo yuko na familia yake, na alikuwa na kijana anayemsaidia kuuza, huku akiwa amehifadhi kwenye begi jeusi alilobeba mgongoni.

Aidha, wananchi waliokuwa kwenye mstari walionekana kuchangamkia bidhaa hizo kwa kila mmoja kutaka kuvaa baji yenye picha ya Dk. Mengi.

Dk. Mengi alifariki dunia Mei 2, mwaka huu Dubai katika Falme za Kiarabu, na mwili wake ulisafirishwa Mei 6, mwaka huu, na kupokelewa JNIA kisha uliagwa katika viwanja wa Karemjee jijini Dar es Salaam Jumanne.

Mwili huo ulisafirishwa Jumatano hadi mkoani Kilimanjaro na kupokelewa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), na baadaye kupelekwa Machame ambako ulilala kwa usiku mmoja na kufanyiwa ibada katikwa Usharika wa Moshi mjini.

Mwili wa Dk. Mengi ulizikwa Mei 9, mwaka huu, katika makaburi ya familia katika kijiji cha Kisereni Kata ya Machame, Wilaya ya Hai.



Baadhi ya akinamama kutoka Wilaya ya Serengeti, mkoani Mara, wakiangalia kuku wanaofugwa kwenye shamba la Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, eneo la Zuzu, jijini Dodoma jana, walipofika hapo kujifunza shamba darasa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mvua kubwa mfululizo zaja

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA),imesema mvua za mfululizo katika baadhi ya maeneo ya Pwani ya Kaskazini katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga zitaendelea kunyesha hadi kesho, huku zikiwa zimesababisha eneo la Jangwani kufungwa kwa muda.

Mvua hizo ambazo ni muendelezo wa masika zimeendelea kunyesha maeneo mbalimbali na kusababisha madhara kama mafuriko katika makazi ya watu na eneo la Jangwani ambako mabasi ya mwendokasi yanapita kwenda na kurudi katikati ya jiji kufungwa kwa muda.

Meneja wa Kituo Kikuu Utabiri wa Hali ya Hewa (TMA), Samuel Mbuya, alisema mvua hizo zinazoendelea kunyesha maeneo ya Pwani ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki na Kanda ya Ziwa Victoria ni sehemu ya mvua za Masika.

"Mvua hizi zinatokana na kuimarika kwa ukanda wa mvua (ITCZ), na mvua mfululizo katika baadhi ya maeneo ya Pwani ya Kaskazini katika mikoa ya Tanga, Dar es Salaam na Pwani pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba zinatarajiwa kuendelea kwa siku mbili mfululizo hadi kesho Jumapili," alisema Mbuya.

Alisema pia vipindi vya mvua za mfululizo vinatarajiwa kujirudia kuanzia katikati ya mwezi huu na kuahidi kuendelea kutoa taarifa za mwenendo wa mvua hizo.

Aidha, TMA iliwatahadharisha wakazi wa maeneo yaliyotajwa, kuendelea kufuatilia taarifa za utabiri wa hali ya hewa na kuzingatia tahadhari zilizotolewa, kuzingatia ushauri na miongozo ya wataalam katika sekta husika ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

"Pamoja na kwamba mvua za masika zinatarajiwa kupungua katika maeneo mengi mwishoni mwa mwezi huu, athari za mvua kubwa zilizonyesha kwa wiki moja mfululizo katika ukanda wa Pwani ya Kaskazini pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba zimesababisha kutuama kwa maji na mafuriko," alisema Mbuya.

Alisema kutokana na ardhi kuwa na unyevunyevu mwingi, ongezeko kidogo la mvua linaweza kuendelea kusababisha athari kama zilizojitokeza hivyo wananchi wanapaswa kuchukua tahadhari.

**BARABARA YAFUNGWA**

Katika eneo la Jangwani unakopita mto Msimbazi, maji yalijaa usawa wa daraja na kusababisha magari kushindwa kupita, hivyo Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (Udart), kulazimika kuifunga kwa muda.

Ofisa Uhusiano wa Udart, Deus Buganywa, akizungumza na Nipashe kuhusu kufungwa kwa barabara hiyo, alisema ni baada ya maji kufika usawa wa barabara hivyo kuhofia kuleta athari kwa vyombo vya moto na watumiaji.

"Leo (jana) saa 5:40 asubuhi, tumelazimika kufunga barabara kwa muda hadi saa 7:10 mchana, tukafungua kwa

INAENDELEA UK. 8

# Pinda atoa neno uwekezaji wa China Afrika

**Na Sabato Kasika**

WAZIRI Mkuu Msaafu, Mizengo Pinda, amepongeza jitihada zinazofanywa na China kuwekeza na kufanya biashara barani Afrika, ikiwamo kusimamia miradi mikubwa ya ujenzi.

Pinda ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye hafla ya uzinduzi wa kinywaji cha pombe kiitwacho Kweichow Moutai kinachotengenezwa nchini China, alitoa pongezi hizo juzi jijini Dar es Salaam.

"Lengo lao ni kutangaza biashara zao na kuendeleza mahusiano kati ya Tanzania na China kwa kuzingatia kwamba urafiki wetu ni wa muda mrefu, wamejenga kiwanda cha Urafiki, treli ya Tazara na pia wana kampuni mengi nchini ambayo yameajiri Watanzani... ninawapongeza sana," Pinda alisema.

Alisema mwezi ujao Tanzania inatarajia kupata watalii 343 kutoka China, na kwamba hatua hiyo itaifanya nchi hii kupata fedha za kigeni na hivyo kuna haja ya kutafuta kila njia ya kushirikiana nao.

"China ni taifa la pili duniani kiuchumi, hivyo ushirikiano uliopo kati yake na Tanzania utakuwa ni daraja la kupata faida kama taifa na hasa kupitia utalii, kwani tunatamani kila baada ya wiki litatua kundi moja la watalii, lengo ni kutaka idadi yao ifikie 10,000," alisema.

Naye Mjumbe wa bodi na Naibu Katibu wa Bodi ya Moutai, Wang Yan, alisema miaka 40 iliyopita nchi ya China ilikuwa miongoni mwa mataifa maskini duniani kuliko umaskini uliopo katika baadhi ya nchi za Afrika.

Alisema hayo wakati wa majadiliano ya biashara ya juu na kufafanua kuwa kwa sasa makampuni yaliyoanzishwa nchini humo yamefanikiwa kubadili mfumo wa maisha ya wananchi wa China na kupata mafanikio makubwa ya kibiashara na kuchangia kuleta maendeleo ya nchi kwa haraka.

"Kama Moutai, tumechagua Afrika kutokana na kuwa na ushirikiano mzuri katika kipindi kizuri kilichopita na ushirikiano huu unaonekana utazidi kuimarika katika siku zijazo na kuongeza mafanikio," alisema Yan.

Alisema chapa ya kinywaji cha Maotai kutokana na umaarufu wake kimekuwa kikitumiwa na watu wengi na kina hadhi kubwa kama zilivyo chapa kubwa duniani kama vile WPP, Kantar Millward Brown, Forbes na Financial Times.

"Kama vile nchini China, watu hapa wanapenda pombe nzuri au divai kwa sababu huleta furaha. Pia tuna matumaini kwamba kuwasili kwa Moutai kutaleta furaha zaidi kwa watu wa Tanzania, hivyo ninatangaza rasmi kuanzia sasa kinywaji hiki kitapatikana katika soko la Tanzania," alisema.

Hafla ya uzinduzi wa kinywaji hicho ilihudhuriwa na wageni wa aina mbalimbali ikiwamo Waziri Mkuu Mstaafu, John Malecela, wanadiplomasia, viongozi wa serikali, maofisa waandamizi wa wa serikali na wawakilishi wa makampuni ya biashara na taasisi za kukuza utamaduni wa China na Tanzania.

# 'Changamkieni fursa za bomba la mafuta'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa utekelezaji wa programu ya kuwashirikisha wananchi (local content) wa mikoa minane inayopitiwa na mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga umeanza, ikiwataka wananchi kutumia fursa mbalimbali za mradi huo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana na Ajira na Wenye Ulamavu, Jenista Mhagama, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Msalala, Ezekiel Maige (CCM).

Katika swali lake, Maige alisema Serikali ya Tanzania ni mdau wa mradi mkubwa wa bomba hilo na wawekezaji katika mradi huo walishateua eneo la kujenga kiwanda cha kuunganisha na mabomba katika mji mdogo wa Isaka.

"Je, ni hatua gani zimefikiwa katika ujenzi wa kiwanda hicho?" Maige alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri Mhagama alisema tayari wameshaanza kutekeleza programu hiyo kwenye mikoa minane ili wananchi watumie fursa mbalimbali za mradi huo katika kujiletea uchumi.

"Nawasihi wabunge wanaotoka katika mikoa hiyo kushiriki kikamilifu kuwahamasisha wananchi kushiriki kwenye programu hiyo na kujifunza fursa za bomba," alisema.

Mhagama aliongeza: "Mradi wa bomba la mafuta ambalo ni muhimu kwa ajira na uchumi wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu inatekeleza programu ya local content katika mikoa yote minane ili wananchi wetu waweze kutumia fursa za mradi wa bomba la mafuta."

Alisema Ofisi ya Waziri Mkuu imeshatoa mwongozo wa ushirikishwaji wa Watanzania katika miradi ya kimkakati na ambayo ni mikubwa ya kipaumbele ili wananchi wetu watumie fursa za miradi hiyo kujiletea maendeleo.

Alisema mikoa inayonufaika na programu hiyo ambayo wananchi wanahamasishwa kuchangamkia fursa mbalimbali kama sehemu ya uwezeshaji kiuchumi ni Tanga, Kagera, Shinyanga, Geita, Tabora, Singida, Dodoma na Manyara.

Awali, Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akijibu kwa niaba ya Wizara ya Viwanda na Biashara, alisema ujenzi wa kiwanda cha kuunganisha na mabomba utaanza mara tu baada ya kukamilika kwa utaratibu wa kuthaminisha na kutwaa ardhi na kukabidhiwa wakandarasa wa ujenzi.

Alibainisha kwa sasa utaratibu wa utwaaji ardhi uko katika hatua ya mwisho na unatarajia kukamilika mapema Julai mwaka huu.

Pamoja na hayo, alisema mkandarasi anatarajiwa kukabidhiwa eneo la mradi na kupeleka vifaa Septemba mwaka huu.

"Mpango wa usimamizi wa mazingira na jamii umekamilika na kuidhinishwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (Nemc)," alisema.

# Wazee 1,300 wapata neema ya matibabu

**Na Rose Jacob, MWANZA.**

WAZEE 1358 wilayani Nyamagana mkoani Mwanza, ambao wamefikisha umri wa miaka 60 na kuendelea, wamepatiwa vitambulisho vya matibabu, ikiwa ni hatua ya serikali katika kuhakikisha wananchi walio fikisha umri wa kuzeeka wanapata matibabu.

Pia kuhakikisha wanakuwa na afya njema katika kutoa mchango wa mawazo yao ya kimaendeleo katika maeneo wanayoishi.

Vitambulisho hivyo vilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, wakati wa hafla fupi katika Kata ya Mabatini, huku akionya vikali watu ambao hawakidhi vigezo, lakini wanajiingiza katika kundi la wazee kuwa watambue watakapobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

"Serikali ya Rais John Magufuli, imekuwa mstari wa mbele katika kutekeleza sera ya Taifa ya wazee ya mwaka 2003, pamoja na maelekezo yaliyoainishwa kwenye sera ya afya ya mwaka 2007 yenye lengo la kuhakikisha wazee wa Tanzania wanatambulika, kupewa fursa ya kushiriki katika mambo yanayo husu maisha yao, hivyo tuwe waaminifu katika suala hili la matibabu bure," alisema Mongella.

Aidha Mongella, aliwakemea watemdaji walio katika hospitali, zahanati na vituo vya afya kuacha tabia ya kuwanyanyapaa wazee.

Akisoma taarifa ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Editha Ngowi, mratibu wa wazee na watu wenye ulemavu, alisema tangu mwaka 2012 jumla ya vitambulisho 9,126 vimeshagawiwa, na jumla ya wazee 10,193 sawa na asilimia 79 wamepata.

"Upatikanaji na utolewaji wa matibabu kwa wazee umekuwa na changamoto mbali mbali, ambazo halmashauri imekuwa ikizifanyia kazi kwa namna moja...upungufu wa dawa za wazee kwenye vituo vya kutolea huduma na ukosefu wa makazi ya kulelea wazee kwenye wilaya ya Nyamagana," alisema Ngowi.




Mwendesha guta akiwa ameisheheni mzigo wa magodoro, katika Barabara ya Sam Nujoma, eneo la Mwenge, jijini Dar es Salaam juzi, na kumfanya ashindwe kuona nyuma kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# Ajali 28 zatokea milima Sekenke miaka miwili

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya ajali 28 zimetokea katika milima ya Sukamahela na Sekenke mkoani Singida kwa kipindi cha kuanzia Januari 2016 hadi Desemba 2017.

Hayo yalielezwa jana bungeni jana na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuph Masauni, alipojibu swali la Mbunge wa Manyoni Mashariki, Daniel Mtuka (CCM).

Katika swali lake, mbunge huyo alisema kumekuwa na ajali nyingi za kutisha katika milima ya Sekamahela eneo la Mbwasa, Manyoni na Sekenke-Shelui.

"Je, kwa kipindi cha miaka miwili yani Januari 2016 hadi Desemba 2017, ni ajali ngapi zimetokea katika milima tajwa na serikali inatoa tamko gani ili kupunguza au kukomesha kabisa ajali katika maeneo haya ndani ya Mkoa wa Singida," mbunge alihoji.

Akijibu maswali hayo, Masauni alisema katika ajali hizo, watu 33 walipoteza maisha na 26 kujeruhiwa katika kipindi hicho.

Alisema serikali kupitia Jeshi la Polisi inawataka madereva kuwa makini wanapoendesha vyombo vya moto barabarani na wazingatie sheria, kanuni, taratibu, alama na michoro iliyoko barabarani.

"Tunawataka kuzingatia udereva wa kujihami ili kuepusha ajali nyingi zinazotokea katika maeneo hayo zinasababishwa na uzembe wa madereva, ubovu wa magari, uchovu hususani kwenye uwapo kona kali, milima na miteremko mikali," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji kama serikali haioni haja ya kufanya usanifu upya kutokana na magari mengi kudondoka katika eneo hilo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, alisema kuwa kabla ya ujenzi wa barabara, ajali zilikuwa nyingi tofauti na ilivyo sasa.

Alisema wanafanya utafiti na wataweka msukumo kwenye eneo hilo ili wachukue hatua kadri ya upatikanaji wa fedha kutoka serikalini.






# Majaliwa awashauri wawekezaji kuhusu ajira

**INATOKA UK. 2**

mbalimbali vya uwekezaji ikiwamo vya kikodi kupitia timu maalum.

" Kwa sasa tuna uhakika kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia kikao cha Bunge na la bajeti linaloendelea tunaweza kupata ufumbuzi wa vikwazo vya kikodi vilivyojitokeza kwa kipindi kirefu cha uwekezaji wenu," alisema Waziri Mkuu

Aliipongeza TOTAL kwa mafanikio iliyopata na jinsi ambavyo inaona umuhimu wa kushiriki kwenye shughuli za maendeleo ya jamii nchini

"Tangu mwaka 2015, kampuni ya TOTAL imewekeza nchini mtaji mkubwa wa zaidi ya dola za Marekani milioni 200 ili kutoa huduma za uagizaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za mafuta ikiwamo mafuta ya dizeli, petrol, vilainishi mbalimbali pamoja na bidhaa za nishasti mbadala," alisema.

Waziri Mkuu alisema pia kampuni hiyo imekuwa ikichangia shughuli mbalimbali za kijamii ikiwa ni pamoja na kutoa shilingi milioni 25 kila mwaka kwa ajili ya masuala ya usalama barabarani.

Alitaja shughuli nyingine ni ujenzi wa madarasa uliogharimu milioni 45, ujenzi wa vituo vya afya shilingi milioni 80na uchangiaji wa madawati 3,000 kwa baadhi ya shule za Mkoa wa Dar es Salaam.

**INAENDELEA UK. 8**

## HABARI KITAIFA

# Serikali yafafanua tena nyongeza ya mishahara

**Na Agusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, amesema serikali itaendelea kutoa nyongeza ya mwaka ya mshahara kwa watumishi wote kadri uwezo wa kulipa utakavyoruhusu.

Amesema walimu hawapaswi kudai malimbikizo ya nyongeza ya mwaka ya mshahara kwa miaka ambayo nyongeza hiyo haikutolewa.

Waitara alitoa kauli hiyo jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Zainab Mussa Bakar, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema walimu wote nchini wameingia katika mkataba na mwajiri ambao pamoja na mambo mengine, unaonyesha uwapo wa nyongeza ya mshahara kila ifikapo Julai, lakini tangu serikali ya awamu ya tano iingie madarakani, walimu hawajapewa haki hiyo.

Alihoji lini serikali itawalipa walimu nyongeza hiyo ya mshahara kama malimbikizo.

Akijibu swali hilo, Waitara alisema serikali imekuwa ikitekeleza miongozo mbalimbali iliyowekwa kuhusu maslahi ya walimu ikiwa ni pamoja na kutoa nyongeza za mwaka za mishahara.

Alisema nyongeza hiyo imekuwa ikitolewa kulingana na utendaji mzuri wa kazi na kwa kuzingatia tathimini ya utendaji kazi ya kila mwaka.

"Kwa mujibu wa Kanuni E.9(1) ya Kanuni za Kudumu Katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 Toleo la Tatu, nyongeza ya mwaka ya mishahara haipaswi kuombwa au kudaiwa na walimu, bali serikali ndiyo yenye uamuzi wa kutoa au kutotoa nyongeza hiyo kutokana na sera za kibajeti kwa mwaka husika," alisema.

Waitara alisema watumishi wa umma wakiwamo walimu, wanastahili kupewa nyongeza ya mwaka ya mshahara iwapo bajeti ya mishahara inaruhusu.

"Kutokana na ufinyu wa bajeti, nyongeza hii haikutolewa kwa watumishi katika mwaka wa fedha 2003/4, 2004/5, 2008/9, 2011/12, 2012/13, na 2016/17, kwa kutambua utendaji mzuri wa kazi, serikali ya awamu ya tano ilitoa nyongeza ya mwaka ya mishahara kwa watumishi wote wakiwamo walimu katika mwaka 2017/18," alisema.



Mwananchi akiruka nyaya za umeme zilizoanguka katika Barabara ya Mabibo sokoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Acacia yaongeza uzalishaji wa dhahabu

**Na Gwamaka Alipipi**

KAMPUNI ya uchimbaji madini ya Acacia, imesema katika kipindi cha ngwe ya pili ya mwaka uzalishaji wa madini ya dhahabu umeongezeka na kufikia wakia 47,805 kwa mwezi.

Hali hiyo imetokana na mafanikio katika mgodi wa madini wa North Mara ambao umeongeza uzalishaji na kufikia wakia 33,941 ikiwa ni zaidi ya asilimia 54 ya wastani wa uzalishaji wa mwezi kwa awamu ya kwanza.

Taarifa iliyotolewa na Kaimu Afisa Mtendaji Mtendaji Mkuu wa Acacia, Peter Geleta, ilieleza kuwa: "Nina furaha na kuongezeka kwa uzalishaji, tumeongeza uzalishaji zaidi ya matarajio yetu ya mwaka kutoka kipimo cha dhahabu cha wakia 500,000 hadi 550,000."

Alisema Acacia itaendelea kushirikiana na Kampuni ya uchimbaji dhahabu ya Barrick wakati huu wakiendelea kufanya mazungumzo na serikali ya Tanzania.

Alisema kwa mwezi Aprili, uzalishaji ulikuwa kipimo cha dhahabu cha wakia 47,805 ikiwa ni zaidi ya asilimia 37 kwa wastani wa mwezi wakati wa awamu ya kwanza ya mwaka 2019.

Alisema mgodi wa North Mara uzalishaji wa dhahabu kwa mwezi ulikuwa kipimo cha dhahabu cha wakia 33,941, ikiwa ni zaidi ya asilimia 52 kabla ya wastani na asilimia 54 zaidi ya wastani kwa mwezi wakati wa awamu ya kwanza ya mwaka 2019.

Alisema uzalishaji katika mgodi wa Buzwagi ulikuwa ni kipimo cha dhahabu cha wakia10, 705 kwa mwezi ikiwa ni asilimia 12 zaidi ya wastani wa awamu ya kwanza ya mwaka 2019.

UNHCR
The UN Refugee Agency

CALL FOR EXPRESSION OF INTEREST (CEoI)

**Implementation of 2020 UNHCR Refugee Protection and Assistance Projects in Tanzania**

**CEoI - Ref. No: UNHCR/2019/001 – Tanzania; May 2019**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR) was established on December 14, 1950 by the United Nations General Assembly. The agency is mandated to lead and co-ordinate international action to protect refugees and resolve refugee problems worldwide. Its primary purpose is to safeguard the rights and well-being of refugees. It strives to ensure that everyone can exercise the right to seek asylum and find safe refuge in another State, with the option to return home voluntarily, integrate locally or to resettle in a third country. It also has a mandate to help stateless people.

In delivering its mandate, UNHCR also collaborates with more than 900 governmental, non-governmental, UN agencies and other partners, and this partnership is solid and expanding.

While host Governments have the primary responsibility for assuring protection and provision of basic services to refugees and asylum-seekers, UNHCR supports the Governments in discharging this responsibility in line with international protection standards.

UNHCR is physically present in Tanzania and supports the Government of Tanzania in the provision of assistance to refugees and asylum seekers also known as Persons of Concern (PoCs) through close collaboration with the UN-system in Tanzania and through partnership(s) with international / local organization(s) and other stakeholders based in Tanzania.

The purpose of this Call for Expression of Interest (UNHCR/2019/001 - Tanzania) is to solicit interest from existing or prospective partners that wish to participate in the UNHCR operation in Tanzania and contribute complementary resources (human resources, knowledge, funds, in-kind contribution, supplies and or equipment) to achieving common objectives as agreed in a Project Partnership Agreement.

The partners to be selected through this CEoI are expected to manage the daily operational programme activities under UNHCR's overall guidance in line with the UNHCR global and operational strategic priorities, policies, procedures and guidelines.

Organizations that have the required technical and complementary attributes to UNHCR's capacities and resources for undertaking any of the below-mentioned Programme areas are invited to respond to this CEoI (Ref. No: UNHCR 2019/001 - Tanzania) by submitting a Concept Note/s on https://www.unpartnerportal.org latest by 9th June 2019. Registration on the Portal is pre-requisite for submission of concept notes. The Concept Note (one per programme area) must be clear and concise, not exceeding 3 pages and only written in English language. The programme areas are:

1. Health, Nutrition, Reproductive Health and HIV services
2. Water, Sanitation & Hygiene (WASH); Shelter and Infrastructure
3. Resilience, Livelihoods and Self –reliance, Energy and Environment
4. Camp Management including non-food items distributions
5. Education and Youth Empowerment
6. Protection of children, persons of specific needs (PSN), SGBV including Psychosocial and Legal support/assistance
7. Warehousing, Mechanical workshop, Fleet and Fuel maintenance and management
8. Various assistance to refugees and asylum seekers in Dar es Salaam

Concept note template with brief description and background of each programme area and selection criteria can be found on **https://www.unpartnerportal.org.** Upon receipt of the Concept Notes, a UNHCR multi-functional Committee will review the concept notes in accordance with the pre-defined criteria. The applicant organizations will receive written notification of the outcome of the assessment before end of July. Instructions for any follow-up that might be required by the applicants will be provided in this response.

In case of need for clarifications or additional information, please contact **tandaeoi@unhcr.org** **before 20th May 2019.**

Please also consult UNHCR's website www.unhcr.org for more information on UNHCR and its global policy priorities.

National NGOs are strongly encouraged to participate and submit their concept note/s for this important call.

| | |
|---|---|
| Issuing UNHCR Office | Implementing Partnership Management Committee Chairperson. Call for Expression of Interest 2019 |
| Contact Address | P. O. Box 2666, Plot 1658 [illegible] Street, [illegible], Dar es Salaam |
| Signature, Representative | |
| Full name and title, Representative | Ms. Chansa Kapaya, Country Representative |
| Name of UNHCR Office | UNHCR Representation Office, Dar es Salaam |
| Date | 09/05/2019 |

215222202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Viongozi wapya Yanga wanahitaji ushirikiano

**HATIMAYE** baada ya mvutano wa muda mrefu, Klabu ya Yanga imepata uongozi mpya uliopatikana katika uchaguzi mkuu uliofanyika Jumapili iliyopita katika Ukumbi wa Bwalo la Maafisa wa Polisi Oysterbay jijini Dar es Salaam.

Viongozi hao ambao watakuwa na jukumu la kuiongoza Yanga kwa kipindi cha miaka minne ni Mwenyekiti Dk. Mshindo Msolla na Makamu wake, Fredrick Mwakalebela.

Aidha, viongozi hao watakuwa wakifanya kazi kwa karibu na Kamati ya Utendaji iliyochaguliwa siku hiyo ambayo inaundwa na Franck Kamugisha, Arafat Haji, Salum Rupia, Bahati Mwaseba, Saad Kimji, Rogers Gumbo, Ahmad Islam na Dominic Kata.

Kwanza kabisa Nipashe kama wadau wakubwa wa michezo nchini tunaipongeza Yanga kwa kufanya uchaguzi kwa amani na utulivu huku walioshindwa wakikubali matokeo. Huo unaonyesha ndio ukomavu na kukubali demokrasia iliyotumika.

Sisi tunasema huo ndio uanamichezo kama ilivyo mchezo wa soka ambao walikuwa wakiwania nafasi hizo ili kuusimamia ambao una matokeo matatu, kushinda, kushindwa na kutoka sare.

Na kwa bahati nzuri au mbaya katika uchaguzi huo hapakuwa na sare (kulingana kwa kura) na kilichotokea ni kushinda na kushindwa tu. Hata hivyo, uchaguzi sasa umepita na kinachotakiwa ni kuvunja makundi kisha kuwa kitu kimoja katika kuijenga Yanga imara.

Tunafahamu viongozi waliochaguliwa wanahitaji ushirikiano mkubwa kutoka kwa wagombea walioshindwa pamoja na Wanayanga wote.

Aliyekuwa mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti, Tiboroha, ametangaza kuwa tayari kushirikiana na Msolla endapo atahitaji mchango wake kwa sababu yeye bado ni mwanachama halali wa Yanga.

Makamu Mwenyekiti, Yona Kevela, ameonyesha uanamichezo wake kwa kuridhika na matokeo na kuunga mkono viongozi waliochaguliwa huku akiichangia klabu yake hiyo Sh. milioni 20.

Si hivyo tu, Kevela pia ametangaza kuvunja kundi lake la wakati wa kampeni na kuahidi kuendelea kuwa karibu na viongozi waliochaguliwa.

Hicho ndicho kitu Nipashe tunataka kukiona kikiendelea kutokea kwa wagombea wengine walioshindwa kuvunja makundi yao na Wanayanga wote wakiwa kitu kimoja.

Lengo letu ni kutaka kuona Yanga ikihitimisha rasmi kipindi kigumu cha mtikisiko wa kiuchumi inachokipitia na kuimarika kama ambavyo watani wao wa jadi, Simba wanavyoimarika kila uchao.

Hilo litawezekana tu kama walioshindwa watavunja makundi yao na wanachama wote pamoja na mashabiki wa Yanga watakubali kuwa kitu kimoja na uongozi waliouweka madarakani katika kuipigania klabu yao.


Tunatambua uongozi mpya sasa utakaa na kuanza mikakati ya namna ya kutekeleza yale waliyoahidi ili kuweza kuijenga Yanga imara na kuitoa katika hali ngumu inayopitia.

Lakini ili kufanikiwa katika hilo, amani inatakiwa kutawala klabuni huku ushirikiano mkubwa ukihitajika kutoka kwa wanachama wote.

Sote tunatambua kuwa ubora wa timu ya Taifa, Taifa Stars kwa miaka mingi umekuwa ukitokana na kuimarika kwa klabu zote husuan Simba na Yanga, hivyo tunataka kuona ushindani ukirejea kwa klabu hizo mbili ili kuinua soka letu. Tunawatakia kila la kheri viongozi wapya Yanga katika kuijenga upya klabu hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hakuna kapa isiyokuwa na usubi

Na Barnabas Maro

**'USUBI'** ni wadudu wadogo wanaofanana na mbu. 'Kapa' ni sehemu ya pwani inayoota mikoko na ambayo huwa na tope na haikosi usubi. Maana yake hakuna msitu wa mikoko usiokuwa na usubi.

Methali hii yatufunza kuwa hakuna kitu kisichokuwa na kasoro au hitilafu zake. Kila kitu kina faida na hasara zake.

Tangu viongozi waliokuwa madarakani katika utawala uliopita kutangaza kujiuzulu, wanachama na mashabiki wa Yanga walionekana wameshindwa kukubaliana na uamuzi huo. Jambo hilo lilisababisha klabu ya Yanga ishindwe kujiendesha yenyewe hata kuitwa 'ombaomba' (hali duni inayohitaji msaada kutoka kwa wengine).

Watani zetu (Simba) wakawa wanatutania kwa kuituita 'Yanga bakuli' yaani tunaopita na bakuli mitaani na viwanjani kuomba msaada. Hata Yanga ilipokuwa inapambana na timu zingine, wapiga picha za runinga hawakukosa kuonesha picha za watu waliokuwa wakichangisha fedha kwa ajili ya Yanga.

Ilikuwa fedheha ya aina yake kwa klabu kongwe kuomba msaada viwanjani. Ni jambo lililokera wengi, lakini hatukuwa na jinsi ila kukubaliana na hali halisi.

Hata hivyo wahenga walisema: "Hakuna kubwa lisilo ukomo." Maana yake kila jambo lina mwisho wake kwani hata maisha ya binadamu hufikia kikomo chake.

Jumapili iliyopita, wanachama wa Yanga walifanya uchaguzi na kumchagua Dk. Mshindo Msolla kuwa Mwenyekiti kwa kupata kura 1,276 huku mgombea mwenzake wa nafasi hiyo, Dk. Jonas Tiboroha akiambulia kura 60 tu.

Aliyeshinda nafasi ya Makamu Mwenyekiti ni Fredrick Mwakalebela aliyewashinda wagombea wengine watano kwa kupata kura 1,206. Mwakalebela alipata kuwa Katibu Mkuu wa TFF zamani. Walioshinda nafasi za ujumbe ni: Frank Kamugisha, Arafat Haji, Salum Rupia, Bahati Mwaseba, Saad Kimji, Rodgers Gumbo, Ahmad Islam na Dominic Kata.

Viongozi hawa wameitwaa Yanga ikiwa na matatizo mengi yanayohitaji hekima, maarifa na juhudi kubwa kuirejesha pale ilipokuwa zamani. Kama kuna kiongozi aliyechaguliwa kwa lengo la kujinufaisha badala ya kuinufaisha Yanga, ni vema ajiondoe mapema na kuwaachia wenye uchungu na Yanga, wenye lengo la kuitoa kwenye umasikini uliokithiri.

Viongozi wapya wanapaswa kuzingatia mambo makubwa manne. Wahakikishe wanapata hatimiliki (waraka wa kisheria unaompa mhusika haki ya kumiliki ardhi au mali nyingine) iliyo mikononi mwa mtu asiyetaka kuipa klabu. Kama atakataa kuitoa kwa viongozi, ashitakiwe mahakamani ili haki itendeke ili hatimiliki irejeshwe klabuni.

Hatimiliki hiyo itumiwe na viongozi kawa dhamana ya kupata mkopo wa Benki itakayokubali kujenga ile nyumba iliyokuwa makao makuu ya Yanga zamani kwenye makutano ya mitaa ya Mafia/Nyamwezi jijini Dar es Salaam. Jengo hilo laweza kuwa la ghorofa 10 au zaidi, maalum kwa biashara kama hoteli na maduka, likiwemo duka la klabu litakalouza jezi, skafu, vikombe vya chai, glasi na vifaa mbalimbali vya michezo vyenye nembo ya Yanga.

Pili lile ghorofa linalotumika sasa kule Jangwani, lifanyiwe ukarabati mkubwa ili liwe maalum kwa ofisi za viongozi wa klabu na pia malazi ya wachezaji wanapokuwa kambini badala ya kukodi hoteli za watu binafsi kama ilivyozoeleka.

Tatu, viongozi wapya wafute kabisa mpango wa ujenzi wa uwanja wa mpira pale Jangwani kwani ni eneo linalofurika maji wakati wa mvua za masika na vuli. Ni eneo ambalo chini yake kuna bomba kubwa la maji yanayokwenda kwenye Hospitali Kuu ya Rufani Muhimbili. Kwa ufupi wakubaliane na maelezo ya Serikali kuwa eneo lile halifai kujengwa uwanja wa mpira.

Jambo la nne: Viongozi wapya wawaondoe 'makomandoo' kwani ndiwo wanaotumiwa na viongozi 'wachumia tumbo' wanaojitafutia shibe kwa kuinyonya Yanga. 'Makomandoo' hujifanya ndiwo wanaoijua Yanga na kuipenda sana kumbe ndiko wanakoshibia!

Viongozi wapya wasikubali kupokea taarifa za maneno kutoka kwa watangulizi wao bali kila kitu kifanyike kwa maandishi. Ikiwezekana, vitabu vya hesabu vipelekwe kwa wakaguzi ili vikaguliwe kujua fedha zilizoingia, na kazi zilizofanyia. Endapo kutakuwa na shaka, wahusika washitakiwe ili sheria ifuate mkondo wake.

Dk. Msolla na wenzake wafanye juhudi kuifanya Yanga iwe kampuni na kuwa klabu yenye hisa kwani "Hakuna kubwa lisiloshindwa." Maana yake hakuna jambo lisilowezekana. Hutumiwa kumhimiza mtu anayekabiliana na hali ngumu kuwa lazima atafanikiwa hatimaye.

## HABARI PICHANI

# MVUA KUBWA YALETA USUMBUFU JIJINI DAR



Wachuuzi wa karanga na magari yakipita kwa tabu kwenye maji ya mafuriko katika eneo la Jangwani, kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Waendesha bodaboda wakiwa wamekusanyika katika kituo cha mabasi ya mwendokasi cha Magomeni Mapipa, Barabara ya Morogoro jijini Dar es Salaam jana, kwaajili ya kusubiria abiria ili kuwavusha katika eneo la Jangwani, baada ya eneo hilo, kufungwa kutokana mvua kubwa iliyonyesha na kusababisha mafuriko. **PICHA: JOHN BADI**



Gari aina ya Landrover likiwa limeacha njia na kuingia kwenye mtaro katika Barabara ya Madale, kutokana utelezi uliosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOHN BADI**



Barabara ya Morogoro, ikiwa imefungwa katika eneo la Magomeni Mapipa jana, baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha mafuriko katika eneo la Jangwani. **PICHA: JOHN BADI**



Watumiaji wa Barabara ya Morogoro, jana walilazimika kutembea kwa miguu kutokana na daraja la Mbezi Mwisho magari kupishana kwa shida kipidi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Wakazi wa jiji wakiwa wamejizuia na mvua katika kibanda kilichozungukwa na maji yaliyojaa, baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha mafuriko katika eneo la Jangwani, jijini jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## Majaliwa awashauri wawekezaji kuhusu ajira

INATOKA UK. 4

Alisema uwekezaji wa zaidi ya shilingi milioni 200 ili kusaidia wajasiriamali kupitia mpango ujulikanao kama The African Start Upper Challenge, ambapo tayari Watanzania sita wamenufaika na mpango huo kwa kupatiwa zaidi ya shilingi milioni 25 za kuanzisha shughuli mbalimbali za ujasiriamali.

Aliwataka wawekezaji waliohudhuria sherehe hizo, kuangalia fursa nyingine ya uwekezaji zilizopo katika Jiji la Dodoma na kuzitumia ipasavyo.

"Uwekezaji Tanzania umerahisishwa, wawekezaji na wafanyabishara waendelee kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kuzingatia sheria na kujiridhisha kuwa ulipaji kodi unaendelea katika mazingira yaliyo safi,"alisema.

Alitoa wito kwa TOTAL kutumia uwapo wao nchini kuitangaza vyema Tanzania, pamoja na kujitanua kusaka mawakala mikoani,kama vile Mbeya, Tanga na Lindi.

Rais wa TOTAL Africa anayeshughulikia masoko na huduma, Mittelman alisema kampuni hiyo ilianzishwa mwaka 1969, wamekuwa katika uwekezaji hatua ambayo wanaamini inawawezesha pia kushiriki katika kuchangia azma ya Serikali ya ukuzaji wa viwanda. "Tanzania ya Viwanda, tumeitikia wito wa Rais Magufuli wa kuongeza biashara na uwekezaji Tanzania ,TOTAL ni wabia Wakuu (leading partner) kwenye mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta litakalosafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda kuja Tanga Tanzania," alisema Mittelman.

Alisema siku zote wanaamini kuwa uimara wa uhusiano wao na Serikali, hutatokana na uvumilivu na uaminifu wao kwa jamii ya Watanzania.

Alisema wamewekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 200 hasa kwenye ununuzi wa kampuni ya GAPCO, jambo ambalo limetusaidia kutanua mtandao wao mara tatu zaidi na kufikisha vituo zaidi ya 100 vya kuuzia mafuta nchini hapa.

# Mahakama sasa yawaengua wakurugenzi kusimamia uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, jana ilibatilisha kifungu cha sheria cha 7(3) kinachowaruhusu Wakurugenzi wa Manispaa na Halmashauri kuwa wasimamizi wa uchaguzi nchini.

Uamuzi huo ulitolewa na Jaji wa Mahakama Kuu, Utuganile Ngwala, kunatokana na kesi namba nane mwaka 2018 iliyofunguliwa na Bob Chacha Wangwe ambaye ni mwanachama wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Katika maamuzi hayo Jaji Ngwala pia alitengua kifungu cha 7 (1) kinachoruhusu mtu yeyote kuwa msimamizi wa uchaguzi.

Akisoma uamuzi huo, Jaji Ngwala alisema kuwa sheria hizo ni batili na ni kinyume cha katiba ya nchi.

Alisema kwa mujibu wa ushahidi uliowasilishwa kwenye mahakama hiyo na muombaji kuwa wasimamizi wa chaguzi wengi wao ni wanachama wa vyama vya siasa ambao wanamaslahi kwenye uchaguzi.

Kwenye kesi hiyo, muombaji aliwakilishwa na Wakili Fatma Karume ambaye alitoa ushahidi wa majina 74 ya wasimamizi wa uchaguzi ambao ni wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Jaji Ngwala alisema kuwa sheria hizo hazijaelekeza utaratibu wowote wa kuhakiki kuwa wasimamizi hawana maslahi binafsi na uchaguzi. Alisema kuwa sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imekataza mtu yoyote ambaye ni mwanachama wa chama chochote kutoruhusiwa kuwa msimamizi wa Uchaguzi.




Maafisa wa Bonde la Wami/Ruvu pamoja na wajumbe wa jukwaa la watumia maji kutoka sekta mbalimbali, wakipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda cha maji cha Hill Water, Hillary Shoo (kushoto), walipofanya ziara ya kikazi ili kukagua shughuli za kiwanda hicho, eneo la Mapinga, wialayani Bagamoyo, mkoa wa Pwani jana. **PICHA: FRANK MONYO**

# Zitto, mawaziri wachuana vikali

INATOKA UK. 2

tuna makisio ya miradi mikubwa haya ni makosa, tuna SGR, Stiegler's Gauge, miradi yote hii haina maana, 'all the money' (fedha zote) zinaenda nje na huduma yetu ya deni la taifa ni kubwa."

Kauli hiyo ilimwinua kitini Waziri Mpango akiomba kumpa taarifa Zitto, akisema: "Nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Zitto, hapa nimeshika ripoti ya rasmi ya pato la taifa na ukuaji wake za 2018 ambayo iko bayana.

"Growth rate' (kasi ya ukuaji) ya 2013 ilikuwa asilimia 6.8, 2014 ilikuwa asilimia 6.7, 2015 asilimia 6.2, 2016 asilimia 6.9, 2017 asilimia 6.8 na 2018 ilikuwa silimia 6.9, sasa hiyo 'growth rate' iliyoteremka ni ipi? "Kwanini mnatumia taarifa za IMF ambazo hazina ukweli"? Na niliwaambia katika Bunge hili kwamba bado tunazungumza na African Development Bank 'wanaproject' (wanadiria) uchumi wa Tanzania 2019 utakua kwa asilimia 6.8, makadirio ya World Bank (WB) ni asilimia 6.6, sasa hiyo growth rate iliyoteremka ni ipi?" Dk. Mpango alihoji.

Baada ya taarifa hiyo, Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, alimuuliza Zitto kama anaipokea taarifa hiyo na mbunge huyo akasema:

"Naipokea taarifa ya Waziri Mpango, ninachotaka kumwambia; kwanza waziri anajua kwamba mamlaka ya 'economic surveillance' (tathmini ya kiuchumi) ya dunia ni moja, nayo ni IMF na anafahamu kwa sababu amefanya kazi huko. "WB, African Development Bank na hata Wizara yetu ya Fedha makisio wanayoyatumia ni ya IMF, siyo makisio mengine na anafahamu, labda atakataa kwa sababu anaitetea serikali hapa," Zitto alisisitiza.

Kutokana na kauli hiyo ya Zitto, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Kijaji alisimama na kutoa ufafanuzi kuwa matokeo ya kupeleka fedha kwenye sekta ya ujenzi, yanaonekana baada ya muda mrefu.

Baada ya kuruhusiwa kuendelea kuchangia mjadala huo, Zitto alisema: "Kuna tofauti kubwa sana kati ya kasi ya ukuaji wa uchumi na uchumi. Sekta ya ujenzi ni ya pili kwenye kasi ya ukuaji, si ya pili kwenye uchangiaji wa kisekta.

"Lakini pointi yangu hapa, wastani wetu tuliokuwa nao ni asilimia. Dk. Mpango anajua panapokuwa na mdororo wowote wa uchumi, serikali inaingiza fedha kwenye mzunguko.

"Na kwa miaka mitatu iliyopita, tumeingiza Sh. 18.7 trilioni kwenye ujenzi, naomba nijibiwe, hii fedha ambayo tumeipampu, imezalisha viwanda vingapi, ajira za kudumu ngapi, sekta ya kilimo imechochewa vipi? Zitto alihoji.

Awali, Naibu Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango, David Silinde, alisema mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) wenye thamani Dola za Marekani bilioni saba haujaleta mabadiliko yoyote kwenye ukuaji wa uchumi.

Aliishauri serikali kufanya uamuzi upya wa kuwekeza katika miradi ya kuzalisha chuma wa Mchuchuma na Liganga ili malighafi zinazotumika kwenye ujenzi huo wa reli zizalishwe ndani ya nchi.

"Mheshimiwa Naibu Spika, shatuna shida si reli kujengwa, isipokuwa ni namna mambo yanavyofanyika, chuma chote kinachotumika kinatoka China na kidogo ndiyo wanapewa wa ndani, tena wanapewa tenda za kudanganyia tani 1,000, tani 2000, basi.

"Haya ni makosa tumekwishafanya na kama hatujawaza mapema, mradi wa awamu ya pili kutoka Makutupora kwenda Mwanza watu wetu wataambulia patupu.

"Kikubwa ninachoshauri makosa yaliyofanyika yasiendelee kufanyika, Dola bilioni tatu za Marekani zikiwekezwa Mchuchuma, manufaa yake ni makubwa, umeme, madini na chuma kitakachotumika hata kwenye hiyo reli," Silinde alisema.

Katika mjadala huo, Mbunge wa Kaliua, Magdalena Sakaya (CUF), aliitaka serikali kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara zinazoziunganisha wilaya za Mkoa wa Tabora na barabara kuu zinazouunganisha mkoa huo na mikoa mingine ili kurahisisha usafirishaji wa mazao hasa tumbaku inayolimwa kwa wiki mkoani humo.

Alisema makandarasi wa ndani waliopewa zabuni za kutekeleza miradi hiyo wameonyesha udhaifu, hivyo kuna haja serikali kuachana nao na kutoa kazi kwa makandarasi kutoka nje.

## Mvua kubwa mfululizo zaja

INATOKA UK. 3

sababu maji yalifika usawa wa barabara na tukahofia yangesababisha itilafu kwenye mabasi yetu na watumiaji kwa ujumla," alisema Buganywa.

Alisema wakati wamefunga barabara hiyo mabasi yaliyokuwa yanatoka Kimara kwenda Kivukoni na Gerezani, yalikuwa yakiishia eneo la Magomeni Mapipa na magari mengine yanayotoka Kariakoo, Kivukoni na kuelekea Muhimbili yalikuwa yakiendelea kutoa huduma.

Alisema licha ya maji hayo kuwa mengi walifanikiwa kudhibiti mabasi yao na hakukuwa na lililopata itilafu yoyote.

"Kama mvua haitaendelea kunyesha tutaendelea kutoa huduma kama kawaida. Tunashukuru hadi sasa hakuna basi lolote lililopata hitilafu kwa sababu tangu mvua za masika zianze kunyesha hatuyalazi tena eneo la Jangwani," alisema Buganywa.

Naye Kaimu Kamanda wa Polisi, Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Camillius Wambura, alisema kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha mfululizo katika mkoa huo, hakuna madhara yoyote ambayo yameshatokea.

Alisema wanaendelea kufuatilia maeneo mbalimbali kuona kama kuna madhara makubwa ambayo yametokea ili kutoa msaada wa karibu.

Hali ilivyokuwa mtaani

Nipashe ilipita maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam na kushuhudia eneo la Jagwani watu wakitembea kwa miguu kutoka Magomeni mapipa kuelekea kituo cha Faya.

Wengine walikuwa wakitoka kituo cha Faya na kuvuka kwa miguu kuelekea kituo cha Magomeni mapipa kwa ajili ya kuunganisha safari zao.

Madereva wa pikipiki na mabuta walitumia fursa hiyo kuvusha watu kwa kutumia vyombo hivyo kwa gharama ya Sh. 5,00 kwa mtu mmoja hadi 2,000.

Aidha, watu waliokuwa wakivuka kwa miguu walilazimika kuvua viatu na kukanyaga maji hayo yaliyokuwa yamefika usawa wa magoti ya mtu mzima ili kuvuka eneo hilo.

Katika daraja la Mto Ng'ombe linalounganisha eneo la Kijitonyama, Alimaua na Tandale kwa Mtogole, hali ilikuwa mbaya, maji yalipita juu ya daraja na kusababisha kuingia kwenye makazi ya watu.

Eneo lingine ambako maji yalikuwa mengi ni Sinza Uzuri ulikopita mto Ng'ombe maji yalipita juu ya daraja na kusababisha kuingia kwenye makazi ya watu, maduka na sehemu za biashara.

# Nigeria kuridhia Azaki, watu binafsi kufungua kesi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SERIKALI ya Nigeria, imeuhakikisha ujumbe wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR), kuwa itashauriana na mamlaka mbalimbali kuhusu azimio la kuruhusu asasi zisizo za kiserikali na watu binafsi kufungua kesi katika mahakama hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa na Makamu wa Rais wa nchi hiyo, Prof. Yemi Osinbajo, mbele ya ujumbe wa AfCHPR, uliotembelea nchi hiyo kutoka Arusha, hivi karibuni.

Rais wa mahakama hiyo, Jaji Sylvain Oré, ndiye aliongoza ujumbe wa majaji na maafisa wengine katika ziara ya kikazi nchini humo.

Makamu wa Rais alisema, Nigeria imeridhia mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na uanzishwaji wa mahakama hiyo, kwa lengo la kulinda haki za binadamu Afrika.

"Ninapongeza kazi zinazofanywa na AfCHPR kuhusu kulinda haki za binadamu," alisema.

Nigeria iliridhia mkataba wa uanzishwaji wa mahakama hiyo mwaka 2004, lakini bado haijaweka azimio kama inavyotakiwa na Ibara ya 34(6) ya mkataba huo ambao unaruhusu watu binafsi na asasi zisizo za kiserikali (NGOs) kufungua mashauri katika mahakama hiyo.

Aidha, alisema Nigeria imejidhatiti kuimarisha amani na utulivu ukanda wa magharibi na Afrika kwa ujumla.

Kwa upande wake, Rais wa AfCHPR, Jaji Oré, aliishukuru serikali ya Nigerian, kwa makaribisho mazuri ambayo ujumbe wake imeupata.

Ujumbe huo ulifanya mazungumzo na maafisa waandamizi wa serikali na kuendesha semina kwa wadau mbalimbali mjini Abuja kutambulisha kazi na majukumu ya mahakama hiyo.

Miongoni mwa maafisa ambao walifanya mazungumzo nao ni Waziri wa Mambo ya Nje, Geoffrey Onyeama na Mwanasheria Mkuu, Waziri wa Katiba, Abubakar Malami, Tume ya Taifa ya Haki za Binadamu na Rais wa Chama cha Wanasheria cha Nigeria na timu yake.



Wakazi wa Mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wakichagua mihogo na viazi kwa ajili ya futari kwenye kipindi hiki cha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhai juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# EAC yaombwa kutenga asilimia 10 kwa kilimo

**Na Cynthia Mwilolezi**
ARUSHA

WAKULIMA wadogo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), wamewaomba wakuu wa nchi hizo kupitia sheria kwa kila nchi kutenga asilimia 10 ya bajeti ya kilimo, ili waweze kupata mageuzi katika sekta hiyo.

Wakulima hao walitoa ombi hilo jana katika mkutano ulioshirikisha wadau wa kilimo kutoka mashirika mbalimbali ya nchi za EAC ambao walijadili changamoto za pembejeo, ukosefu wa maafisa ugani mashambani pamoja na azimio la Malabo lililowekwa saini na wakulima wadogo kutoka nchi za EAC.

Baadhi ya washiriki hao ambao ni Girukwayo Obed (Burundi), Hakimu Baliraine (Unganda) na Sophia Jumanne (Tanzania) walisema endapo wakuu wa nchi wataridhia na kupitisha azimio moja la kila nchi wanachama wa EAC kutenga bajeti ya kilimo ya asilimia 10 wakulima wadogo wataweza kunufaika na kujikwamua kiuchumi.

Mkulima kutoka Burundi, Obed alisema ingawa nchi ya Burundi imefanikiwa kiasi hicho lakini bado nchi hiyo inakabiliwa na changamoto ya utapiamlo pamoja na lishe kwa watoto na watu wazima kutokana na tabia ya wakulima kuuza mazao yote bila kujiwekea akiba majumbani badala yake hununua chakula.

"Bado wakulima wanatakiwa kuelimishwa kuwa unapolima chakula ni lazima pia uweke akiba na si kuuza chote sababu unasababisha njaa, hivyo tunahitaji kupewa elimu zaidi juu ya umuhimu wa lishe na usalama wa chakula kwa kila kaya," alisema.

Naye, Balirane kutoka Uganda, aliwaomba wakuu hao kupitisha azimio hilo kunufaisha wakulima, kwani ukosefu wa bajeti za kilimo unasababisha wakulima kutonyanyuka kiuchumi badala yake kuwa na hali duni wakati wanapaswa kuwa matajiri sababu anazalisha mazao yanayolisha nchi mbalimbali.

Naye mkulima kutoka Tanzania, Jumanne alisisitiza ni vyema maafisa ugani kuwatembelea wakulima wadogo na kuwapa elimu zaidi ikiwamo upatikanaji wa pembejeo za kilimo, ili waweze kujikwamua kiuchumi badala ya hivi sasa kila mkulima kulima mazao ayatakayo pasipo kujua atavuna au la.

Awali Ofisa Mawasiliano kutoka shirika la ESAFF, Emmanuel Justine, alisema wakulima hao kwa pamoja wamekutana kujadili changamoto zao ikiwamo kuomba wakuu wa nchi kupitisha azimio la Malabo la kutenga asilimia

# Wajasiriamali walilia kisa wawekezaji wa vifungashio

**Na Woinde Shizza,**
ARUSHA

WAJASIRIAMALI wadogo wameiomba serikali kutafuta wawekezaji wa vifungashio na nembo ili kupunguza gharama na usumbufu wa kuviagiza nchini Kenya.

Ombi hilo lilitolewa hivi karibuni na mjasiriamali Annet Kivuyo, wakati wa semina ya wajasiriamali iliyoandaliwa na Shirika la wa Viwango Tanzania (TBS).

Alisema ukosefu wa watengenezaji wa vifungashio na nembo kunawarudisha nyuma katika soko la biashara kwa kuwa wanashindwa kukidhi viwango vya ubora wa kimataifa.

Annet alisema kwa mjasiriamali kukosa vifungashio kunachangia kupunguza soko la bidhaa, kwa sababu vifungashio havipo kwenye ubora unaokubalika.

"Vifungashio bora vya kuvutia bidhaa zetu, ziwe kwenye viwango vyenye ubora, tunaiomba serikali ilishughulikie hili kwa kututafutia mwekezaji wa vifaa hivi muhimu kwetu katika biashara ili tutengeneze bidhaa kama Kenya na tuache kununua kwao," alisema Annet. Alisema Tanzania ina bidhaa nzuri zenye ubora, lakini shida kubwa ni ukosefu wa vifungashio na mashine za kutengeneza nembo zinazozalishwa nchini.

Awali, Mkurugenzi wa TBS, Jabir Abdi, alisema wameamua kufanya mafunzo hayo kwa wafanyabiashara wachakataji wa bidhaa za ngozi ili kuwapatia elimu sahihi juu ya kufikia viwango vya kitaifa.

Alisema lengo ni kuwawezesha wajasiriamali kuwa na bidhaa zenye ubora na kupata soko kirahisi ili wauze bidhaa zao ndani na nje ya nchi.

Jabir alisema kuwa wanatoa elimu hiyo ambayo itawawezesha kupata alama za ubora na kufikia malengo yao, na kwamba kitu pekee kitakachomuezesha mjasiriamali kufikia malengo ni kufuata viwango vya kitaifa.

# Ushirika kujenga ghala la mil. 500/-

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa** LIWALE

CHAMA cha Msingi cha Ushirika Umoja cha mjini Liwale mkoani Lindi, kinatarajia kujenga ghala kubwa lenye uwezo wa kuhifadhi tani 7,000 hadi 10,000 za korosho za wanachama wake na wakulima wengine kutoka vyama mbalimbali vya ushirika wilayani humo.

Mwenyekiti wa chama hicho, Hassan Mpako, ndiye aliyesema hayo kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa Umoja Amcos uliofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita na kufafanua kuwa ujenzi huo utagharimu Sh. milioni 500. "Katika mkutano kuu wa mwaka jana tuliomba ridhaa yenu ili tukope kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa ghala lingine kubwa, ninajulisha kuwa tayari tumepata mkopo na tumeanza kujenga msingi," alisema Mpako.

Mpako alisema ghala la sasa lina uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 za korosho, na kwamba msimu wa 2017/2018, lilipokea tani 17,000 na uliopita likiwa limepokea tani 12,000, ambazo ni nyingi kuliko uwezo wa ghala hilo. Ghala kuu ni mradi mama wa chama chetu na pia ni kitovu cha uchumi wa jamii inayotuzunguka, na umetoa ajira na kuleta mzunguko wa fedha kwenye wilaya yetu ndio maana tunataka kujenga ghala kubwa zaidi," alisema.

"Kama ulivyo utaratibu wetu ni kwamba kila mwanachama ataendelea kukatwa Sh. 20 kwa kila kilo moja ya korosho hadi tutakapomaliza mkopo huu wa Sh. milioni 500," alisema.

Kuhusu ukusanyaji wa korosho msimu uliopita, alisema Umoja Amcos imeshindwa kufikia malengo ambayo ilijiwekea na kukusanya tani 4,825, lakini ikaambulia tani 2,813 tu.

"Sababu kubwa ni kutokana na hali ya hewa kuwa mbaya na upatikanaji wa pembejeo usiozingatia wakati na pia ukosefu wa utaalam wa matumizi sahihi ya dawa zinazotumika kwenye zao la korosho," alisema.




Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda (kulia) na Mjumbe wa bodi ambaye pia ni Naibu Katibu wa Bodi ya Moutai kutoka China, Wang Yan (kushoto) na wasaidizi wao wakishiriki katika uzinduzi wa kinywaji cha Kweichow Moutai juzi jijini Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Angalizo upandaji miti kwenye umeme

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WATANZANIA wamekutakiwa kuwa makini wakati wa upandaji wa miti katika maeneo ambayo hayataingiliana na miundombinu ya umeme ili kuepusha athari ambazo zinaweza kutokea ikiwamo vifo.

Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) Mkoa wa Kilimanjaro, Mhandisi Mahawa Mkaka, aliwataka wananchi kuacha tabia ya kupanda miti karibu na miundombinu ya umeme ili kupunguza adha zinazoweza kujitokeza nyakati za mvua.

Mhandisi Mkaka alisema Watanzania wengi hawana elimu ya kutosha juu ya upandaji wa miti na badala yake wamekuwa wakiipanda karibu na miundombinu ya umeme, jambo ambalo limekuwa likisababisha madhara na hata vifo.

"Miti iliyopandwa na kuingilia miundombinu ya umeme imekuwa ikileta athari kwa wanadamu mbali na kusababisha athari zingine zinazohusiana na usambazaji wa nishati hiyo muhimu," alisema na kuendelea:

"Kwa hali hii shirika limelazimika kukata baadhi ya miti ingawa kwa shingo upande kutokana na ukweli kwamba dunia ya sasa inalenga kuboresha mazingira... lakini sisi tumeangalia maslahi mapana na athari zinazoweza kutokana na kuwapo kwa miti pembezoni mwa miundombinu ya umeme."

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, alilipongeza Tanesco kwa uamuzi wake huo, ambapo alisema haunabudi kuigwa na taasisi nyingine za umma zikiwa ni hatua ya kuhakikisha wanairudisha Kilimanjaro katika hali yake ya mwanzo na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Mmefanya vyema katika kuhakikisha zoezi la upandaji miti linaendelea hasa nyakati hizi za masika na tunaomba halmashauri kuhakikisha wanasimamia sheria ndogo ndogo za upandaji wa miti na mifugo pamoja na kutoa elimu kwa wananchi juu ya njia bora za upandaji wa miti bila kuigusa miundombinu ya umeme na vyanzo vya maji," alisema.

Mkazi wa Manispaa ya Moshi, Adelaida Munishi, alisema ni vyema Tanesco kutumia wataalamu wake na kushirikiana na serikali kuhakikisha msimu huu wa mvua wananchi wanapanda miti mingi zaidi kwa utaratibu maalumu.

# Wataka elimu ya saratani tezi dume

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANANCHI wa Mkoa wa Kilimanjaro wameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuendelea kutoa elimu juu ya saratani ya tenzi dume ili kuhakikisha wanaume wanajitokeza kwa wingi katika kupima afya zao.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, Elikana Rafaeli, alisema bado wananchi hawana elimu ya kutosha juu saratani ya tenzi dume hali inayowafanya kuchelewa kufika kwenye matibabu na wakati mwengine kupoteza maisha.

Alisema bado katika jamii kuna imani potofu juu ya ugonjwa wa tenzi dume, hali ambayo serikali ikiingilia kati katika kutoa elimu katika kila mikutano ya vijiji, kata na viongozi wa dini watumie nafasi zao vyema elimu itaweza kufika kwa wakati. "Tunaiomba serikali kutoa agizo kwa wataalamu kwanzia ngazi za vijiji kufika kwa kila mkutano wa kijiji kata wilaya na hata mkoa kutoa elimu ya afya ya kuzungunzia magonjwa ya saratani hasa tenzi dume ili kuleta afueni kwa wanaume," alisema na kuongeza:

"Ikiwa viongozi wa vijiji, tarafa, kata, wilaya na mkoa watapewa agizo la kuhakikisha wanaweka agenda ya afya katika mikutano yao ambapo halmashauri itume mtaalamu wa afya kufika na kuelezea magonjwa ya saratani itasaidia kubadilisha maisha ya Watanzania na kupata taifa la watu wenye afya bora ambapo wataweza kuleta maendeleo."

Grace Lucas ni mkazi wa wilaya ya Siha, alisema katika baadhi ya makabila wamekuwa wakiogopa kwenda kupima na hata wakigundulika kuwa na saratani hiyo wamekuwa wakikaidi kutumia dawa, hali ambayo imekuwa chanzo cha vifo vya mara kwa mara kwa wanaume

Kwa upande wake daktari bingwa wa magonjwa ya saratani ya tenzi dume katika Hospitali ya Rufaa ya KCMC, Necolus Ngowi, alisema bado muamko ni mdogo kwa jamii, hivyo ikiwa serikali italichukulia hilo kama ajenda kuu katika mikutano yake tutaweza kuisaidia jamii ya Watanzania. Alisema watu wanaopata ugonjwa huo mara nyingi ni wanaume wenye umri kuanzia miaka 40 ikiwa katika familia yao kuna ugonjwa huo na 50 ikiwa kwenye ukoo huo hakuna historia ya ugonjwa huo.

"Ni kweli kuwa muamko bado ni mdogo, wananchi hawana elimu ya kutosha, lakini kwa kushirikiana na serikali na mashirika binafsi tutaweza kuwasaidia wanaume wengi na kuokoa maisha yao kwa kuwa saratani yoyote ikiwahiwa inatibika," alisema Dk. Ngowi.

Mkurugenzi wa KCMC Dk. Gileard Masenga, alisema kwa kuona umuimu wa wananchi kupata matibabu na kuchekiwa afya zao, hospitali hiyo iliamua kufungua kituo cha kupima saratani vipimo vya awali ili kunusuru wananchi, hivyo wafike kwa ajili ya kufanya vipimo vya awali. "Wananchi, Hospitali ya Rufaa ya KCMC imefungua kitengo cha uchunguzi wa awali ili kuwanausuru wananchi... wanaume msiogope fikeni kwa wingi," alisema na kuongeza:

"Serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na wanasiasa ikiwa watafanya ajenga hii kuwa muhimu itaweza kuwasaidia wananchi kupata elimu na kuondokana na dhana potofu."








Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, akikagua gari aina ya Noha T732 DFG iliyotumbukia mtaroni inayodaiwa kujeruhi wafanyabiashara wadogo wadogo (wamachinga), waliokuwa wamepanga biashara zao katika eneo la Uhindini jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# Madereva 740 wabainika kutumia kilevi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KIKOSI cha Usalama Barabarani mkoani Dodoma, kimesema katika kipindi cha Januari hadi Septemba mwaka jana, madereva 740 kati ya 1,420 walibainika kutumia kilevi wakiwa wanaendesha vyombo vya moto.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa kikosi hicho, Nuru Selemani, katika ufunguzi wa mafunzo kwa waandishi wa habari 12 za usalama barabarani kwa mwaka 2019/20, jijini hapa.

Mafunzo hayo yameandaliwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yameenda sambamba na maadhimisho ya wiki ya kimataifa ya usalama barabarani ambayo huadhimishwa kila ifikapo Mei 6-12, kila mwaka.

Akizungumza katika mafunzo hapo, Selemani alisema kati yao madereva 540 waliandikiwa faini.

Aidha, alisema madereva 80 wa pikipiki walifungiwa leseni zao baada ya kupelekwa mahakamani na kupatikana na hatia. “Ulevi ni moja ya sababu kubwa sana ya ajali za barabarani kwa mwaka huu tumejipanga kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya vifaa tulivyo navyo kama speed rader na vipima ulevi,” alisema.

Pamoja na hayo, Mkuu huyo alisema katika kipindi cha Januari hadi Aprili mwaka huu, magari 21,905 yalikamatwa na kulipa faini kiasi cha Sh. bilioni 1.05 huku pikipiki 9,200 zililipa faini ya Sh. milioni 276.

Akizungumzia utoaji elimu kwa madereva na wananchi, Selemani alisema jumla ya madereva 34,640 na abiria 1,245,786 walipatiwa elimu ya usalama barabarani.

Kuhusu hali ya usalama barabarani, Mkuu huyo alisema katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka jana ajali 350 zilitokea ambazo zilihusisha magari 155 na pikipiki 195 na kusababisha vifo vya watu 60.

“Katika kipindi cha Januari hadi Aprili 2019 jumla ya ajali 75 zilitokea na kusababisha vifo vya watu 13,” alisema.

Selemani alisema changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni baadhi ya waendesha pikipiki kutofuata taratibu, kanuni na sheria za usalama barabarani kwa kuogopa zaidi askari badala ya kufuata sheria zinazowaongoza. Alieleza kuwa kumekuwapo na jitihada mbalimbali za kupunguza ajali ikiwamo ukamataji wa makosa ya usalama barabarani, kutoa elimu kwa makundi yote ya watumiaji barabara. Naye, Mwenyekiti wa mtandao wa wabunge ambao ni mabalozi wa usalama barabarani, Balozi Adadi Rajabu, alisema zinahitajika jitihada za ziada kwenye kupunguza tatizo la ajali nchini ili kufikia ziro kama ilivyo nchini Sweden.

“Marekebisho ya Sheria ya Usalama barabarani ya mwaka 1973 ambayo ina mapungufu mbalimbali ipo kwenye hatua za mwisho ambapo tunasubiri serikali ikamilishe ilete muswada huo bungeni,” alisema.

Mafunzo hayo ni mwendelezo wa mradi wa ‘Bloomberg Global Road Safety Initiative Tanzania Project’ ambao umejikita kuboresha usimamizi wa mabadiliko ya sheria ya usalama barabarani na kuwawezesha wanasheria na waandishi wa habari kuhamasisha usalama barabarani katika ngazi mbalimbali.

# Shamba la ‘Mtoto wa Mkulima’ laendelea kuwa darasa kivutio

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SHAMBA la Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, limeendelea kuwa kivutio kwa wananchi na makundi mbalimbali kufika na kujifunza.

Hayo yamebainishwa jana na Mtoto wa waziri mkuu mstaafu huyo Peter Pinda, alipokuwa akizungumza na kinamama kutoka Wilaya ya Serengeti mkoani Mara walipofika kujifunza shughuli za kilimo katika shamba hilo lililopo eneo la Zuzu.

Pinda alisema kuna makundi mengi ya wananchi wanaofika katika eneo hilo kila siku kujifunza kuhusu miradi ya kilimo.

“Hapa kuna watu wengi na makundi mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi...wamekuwa wakifika kujifunza shughuli za kilimo hapa, hatuwezi kuwazuia kwa sababu wanavutiwa na aina ya shamba lilivyo,” alisema.

Alisema katika shamba hilo kuna aina mbalimbali za ufugaji ikiwamo ufugaji kuku, ng’ombe wa maziwa na nyama, samaki, mbuzi, kondoo na ufugaji nyuki.

Aliongeza ndani ya eneo hilo kuna kilimo kilimo cha zao la alizeti, mahindi, mbogamboga na mazao mengine mchanganyiko. Mmoja wa kinamama kutoka Serengeti, Pendo Machaba, alisema wao kama wajasirimali wamejifunza mengi kuhusu aina za kilimo na ufugaji kinachofanyika hapo.

Machaba alimshukuru Mbunge wa viti Maalum mkoa wa Mara, Agnes Marwa, kwa kuwawezesha katika ziara hiyo ya mafunzo ya shamba darasa.

“Sisi tumevutiwa sana na shughuli zinazofanyika hapa kwenye shamba la mtoto wa mkulima, tulikuwa tukimsikia akizungumza kwenye majukwaa kuhusu kilimo hatukujua kuwa aliyasemea maisha yake halisi, kweli leo tumeamini,” alisema.

Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mara, Agnes Marwa, alisema mafunzo hayo kwa kinamama hao ni sehemu ya ahadi zake alizowaahidi kuhusu kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali ndani na nje ya Mkoa.

Marwa alisema atahakikisha kuwa atapeleka baadhi ya kinamama kutoka kila wilaya za Mkoa huo kwa awamu ili kujifunza kwa vitendo masomo ya shamba darasa na wao wakirudi watawafundisha wengine na kuweza kuinua uchumi wa familia zao.

# Mikoa mitatu tishio Dengue

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UGONJWA wa homa ya Dengue umewapata watu 1,237 wa mikoa mitatu kwa kipindi cha miezi mitano.

Kwa mujibu wa Mganga Mkuu wa serikali, Prof. Muhammad Kambi, wagonjwa 1,150 ni wa Dar es Salaam, Tanga ina 86 na mmoja Singida.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, alisema idadi ya wanaoambukizwa kila mkoa kwenye mabano iliongezeka na kuwa January (56), Februali (82), Machi (159) na Aprili (940).

Aidha, alisema hadi sasa kuna vifo vya watu wawili na kwamba licha ya ugonjwa huo pia walikuwa na maradhi mengine.

“Naomba wananchi mjitahidi kuchukua tahadhali za ugonjwa huo kwa sababu ni mbaya sana,” alisema Prof. Muhammad.

Akielezea jinsi ya kujikinga na ugonjwa huo, alisema ni kufukia madimbwi ya maji yanayotuama au kunyunyizia dawa ya kuuwa viluwiluwi vya mbu, kuondoa vitu vinavyoweza kuweka mazalio ya mbu, kufyeka vichaka vilivyo karibu na makazi ya watu.

Nyingine ni kuzuia ni kuhakikisha maua yanayopandwa kwenye makopo au ndo haziruhusu maji kutuama, kufunika mashimo ya maji taka kwa mfuniko imara na kusafisha hata za paa la nyumba ili kutoruhusu maji kutuama.

Aidha, alisema mbinu nyingine ni kuvaa nguo ndefu ili kujikinga kuumwa na mbu, kutumia vyandarua vyenye viuatilifu, kutumia dawa za kufukuza mbu na kuweka nyavu kwenye madirisha na milango ya nyumba za kuishi.

Mganga huyo alizitaja dalili za ugonjwa huo kuwa ni homa ya ghafla, kuumwa kichwa hususani sehemu za macho na maumivu ya viungo kwa ujumla.

Prof. Muhammad alisema dalili hizo huanza kujitokeza kuanzia siku tatu hadi 14 mtu anapoambukizwa ugonjwa huo na zinaweza kufanana na za malaria.

Alisema kutokana na hilo wananchi wanapaswa kuwa makini pindi wapatapo homa kwa kwenda kupata huduma kwenye vituo mbali mbali vya afya ili waweze kuchunguzwa kupimwa na kupatiwa matibabu. Alisema mgonjwa wa Dengue anaweza kutokwa na damu sehemu za fizi, midomoni, puani kwenye macho na kwenye njia ya haja ndogo na kubwa.

Kwa mujibu wa Mganga huyo, serikali kupitia Halmashauri za mikoa na wilaya zake inaendelea kuchukua tahadhali ya kuzuia ugonjwa huo ikiwemo kuangamiza mazalia ya mbu.

Mapema wiki hii, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Yudas Ndugile, alisema kuna wagonjwa 1,200 jijini humo na mmoja amefariki. Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari na kujilinda.





# Waliohusika kashfa ya mitihani watimuliwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATUMISHI waliohusika katika kashfa ya uvujaji wa mitihani ya kidato cha pili iliyofanyika Disemba mwaka jana, na Serikali kuifuta wamesimamishwa kazi.

Watendaji hao ni kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na watendaji wa Wizara ya Habari na wamesimamishwa kazi kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma.

Hayo yalielezwa na Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, katika kikao cha bajeti 2019/2020 katika Baraza la Wawakilishi.

Alisema sakata hilo halivumiliki na kuifanya Serikali kuiagiza kamati ya taifa ya ulinzi na usalama kufanya uchunguzi wa kina na kujua chanzo chake, na tayari imeshakamilisha kazi yake na kuiwasilisha rasmi taarifa hiyo serikalini. Alisema taarifa hiyo ya uchunguzi imebaini baadhi ya watendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na baadhi ya watendaji wa wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kubainika kuhusika na kashfa hiyo iliyolitia aibu taifa.

Balozi Iddi alisema Serikali imeshalitaka Jeshi la Polisi kuwachukulia hatua za kisheria kwa mujibu wa makosa waliyofanya wale wote waliohusika na tukio hilo.

Aidha, alisema Serikali inaendelea kuchukuwa hatua katika kuhakikisha mazingira ya elimu yanakuwa mazuri ili watoto wa Zanzibar waweze kupata haki yao ya elimu bila ya malipo.

Alisema inapendeza kuona asilimia ya uandikishaji katika ngazi zote za elimu ya lazima imeongezeka ikilinganishwa na mwaka wa fedha wa 2017/2018 ambapo ngazi ya maandalizi uandikishaji umefikia asilimia 69.4 mwaka 2018 kutoka asilimia 66.1 mwaka 2017. Balozi Iddi alieleza kwamba kasi hiyo ya uandikishaji inatokana na upatikanaji wa nafasi, mwamko wa jamii kuhusu elimu na ushiriki mzuri wa wananchi katika kuleta maendeleo kwenye sekta ya elimu.

Alieleza kwamba katika juhudi za kuimarisha sekta hiyo muhimu kwa taifa lolote lile Serikali ya Zanzibar kwa kushirikiana na mfuko wa (OPEC) imekamilisha ujenzi wa shule tisa za ghorofa za sekondari Unguja na Pemba.

Alisema mradi huo mkubwa umekwenda sambamba na ujenzi wa maabara, maktaba na vyumba vya kompyuta kwa Shule 24 za Sekondari kwa ushirikiano na Benki ya Dunia.

Hata hivyo Balozi Seif Iddi ameliomba baraza la wawakilishi liidhinishe jumla ya Sh. 57,911,349,000 kwa Ofisi yake na taasisi zake kwa ajili ya kutekeleza programu 11 kwa mwaka wa fedha 2019/2020.



Baadhi ya Manaibu Mawaziri wa Wizara za Serikali wakifuatilia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wawakilishi wataka ofisi za ZEC kupewa hadhi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi, wameitaka Serikali kuimarisha ofisi za Tume ya uchaguzi (ZEC) ziliopo wilayani ambazo baadhi yake hazina hadhi, huku zikiwa katika majengo ya mkuu wa wilaya.

Hayo yalisemwa na Mwakilishi wa Jimbo la Ole Pemba, Mussa Ali Mussa, wakati akichangia bajeti ya wizara ya nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Mussa alisema Ofisi za ZEC ni muhimu ambazo zinahitaji usiri mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yake ya kazi. "Kwa mfano, ofisi za tume ya uchaguzi zilizopo Mahonda zipo katika jengo la Mkuu wilaya hiyo," alisema. Aidha lisema ofisi nyingine za ZEC ambazo hazipo vizuri huku zikikosa ufahari mkubwa ni Chake Chake Pemba na Mkoani Pemba. "Mheshimiwa Spika ni kweli Ofisi za Tume ya uchaguzi zilizopo wilayani majengo yake hayana ubora wa sifa za taasisi hiyo ambapo pia zipo katika Ofisi nyengine na hivyo kuhatarisha ufanisi wa majukumu yake," alisema. Naye Mwakilishi wa Chake Chake Pemba, Suleiman Sarhani, aliitaka ZEC kujipanga vizuri kwa ajili ya harakati za uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwakani.

Aliitaka tume kujipanga vizuri na kuhakikisha kasoro zilizojitokeza katika uchaguzi uliopita hazijitokezi tena.

Akijibu hoja za wajumbe wa Baraza hilo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohammed Aboud, alisema upo mradi wa kuimarisha ofisi za uchaguzi wilayani.

Aboud alikiri kwamba ofisi ya ZEC iliopo Wete Pemba ipo katika mazingira ya hatari na kutisha wakati wa uchaguzi mkuu.

"Tumeanza kufanya mawasiliano na Wizara ya Fedha na Mipango kuona Ofisi ziliopo wilayani zinafanyiwa ukarabati mkubwa ili wafanyakazi wetu wafanye kazi katika mazingira mazuri," alisema.

## SMZ kufanyia utafiti mchanga

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema inafanya utafiti wa kujua kiwango cha mahitaji halisi ya rasilimali ya mchanga pamoja na matumizi yake kwa ujumla.

Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, wakati akijibu baadhi ya hoja na michango iliyotolewa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao walitaka kupata ufafanuzi wa hali halisi ya rasilimali ya mchanga.

Mjawiri alisema umakini mkubwa unahitajika katika matumizi ya rasilimali ya mchanga kutokana na ukweli kwamba matumizi ya mchanga ni makubwa tofauti na hali halisi ya upatikanaji wake.

Alizitaja juhudi zilizochukuliwa kwa sasa ni pamoja na kuweka utaratibu mzuri kwa wananchi katika kupata mchanga ikiwamo kuwasilisha maombi ya mchanga kupitia kwa viongozi wa shehia.

Alisema utaratibu huo kwa muda mfupi imebainika umeleta mafanikio makubwa ambapo kwa sasa kwa siku mchanga unachotwa tani 1000 kutoka tani 3,000.

"Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba tumefanikiwa kudhibiti uchotaji wa mchanga katika mashimo yaliyotengwa rasmi ambapo kwa siku kiwango chake ni wastani 1000 kutoka matumizi ya tani 3,000 kwa siku," alisema.

Alieleza hadi sasa hakuna sababu ya kuagiza mchango kutoka nje ya nchi ambapo kama ikilazimika, utafiti zaidi wa kisayansi unahitajika.

Alisema huwezi kuchukuwa mchanga kutoka sehemu nyingine na kuuleta nchini bila ya kufanya utafiti wa kisayansi kwa sababu yapo maradhi yanayotokana na mchanganyiko wa mchanga.

"Utafiti pekee ndiyo utakaotufanya kuagiza mchanga nje ya nchi kwa ajili ya mahitaji yetu...huwezi kuingiza mchanga nje ya nchi bila ya kuufanyia utafiti wa kisayansi'," alisema.


Hata hivyo, alikiri uhaba wa mchanga kwa kiasi kikubwa umetishia kuzorota kwa miradi mikubwa inayotekelezwa na washirika wa maendeleo ikiwamo ya Wizara ya Elimu.



**BANANA** Soma UK.15

BURUDANI TELE

JUMAMOSI MEI 11, 2019



# MENGI
## KWANGU ALIKUWA BABA - BARNABA

Soma UK.14

## BASI SAWA



## Monalisa haamini kama Dk. Mengi hayupo

MSANII mkongwe wa filamu, Monalisa amesema itamchukua muda mrefu kuamini kwamba Dk Reginald Mengi amekufa, kwa vile kifo chake kimekuwa cha ghafla sana.

"Yaani ni kama siamini kweli Mengi amekufa! Lakini kikubwa ni kwamba tuendelee kumuombea kwa Mungu ili apumzike kwa amani mzee wetu, ametufanyia mambo mengi mazuri," amesema Monalisa.

Amesema ajira yake ya kwanza aliipata katika vituo vya ITV na Radio One na pia umaarufu wake katika sanaa aliupata kupitia ITV, hivyo kifo hicho kimemgusa sana na kumkumbusha alikotokea hadi sasa alipo.



## 'Jipe Moyo' yamkumbusha Madam Flora

MWIMBAJI wa nyimbo za Injili, Madam Flora amefunguka kwamba ataendelea kumkumbuka Dk. Reginald Mengi kupitia albamu yake ya kwanza ya 'Jipe Moyo' kwa vile ndiye aliyeizindua.

Amesema wakati anazindua albamu hiyo mjini Moshi mkoani Kilimanjaro mwaka 2005, alimwalika Dk.Mengi kuwa mgeni rasmi na alikubali ombi hilo bila kipingamizi chochote.

"Siyo kukubali mwaliko tu bali pia nilipata nafasi ya kutangaza uzinduzi huo kwenye vyombo vyake bila malipo na nilitokea kumheshimu sana na ninaamini alikuwa anaongozwa na roho wa Mungu, kwani amefanya mambo makubwa kwa Watanzania wengi," amesema Flora.



# MENGI

## KWANGU ALIKUWA BABA - BARNABA

MSANII nyota wa muziki wa kizazi kipya, Barnaba ameguswa na kifo cha aliyekuwa mwenyekiti wa makampuni ya IPP, Reginald Mengi na kusema alimchukulia kama baba yake kwa jinsi alivyokuwa akiijali jamii.

"Ukitaka kujua kile ninachokisema, sikiliza wimbo wangu wa 'RIP Baba' jinsi nilivyomuelezea mzee Mengi...kwa kifupi niseme tu kwamba wema hawana maisha," amesema Barnaba.

Amesema Mengi alikuwa anapenda kukuza sanaa kupitia vyombo vyake vya habari na pia kuwapa vijana ajira bila ubaguzi, ndio maana alikuwa akimuitwa kwa jina la baba kama ilivyokuwa kwa Ruge Mutahaba.

## INSTA-TWITTER





Mwili wote huu anasubiria kufuturu kwa shemeji yake. Na ndiyo kwanza hata 10 la kwanza bado, na dada bado hajaolewa "NI WIVU TU"-**Billnas.**



Humu duniani tunamoishi hakuna binadamu aliyekamilika, wewe unayehisi muda wote uko sahihi kuna wengine wanaona kuishi na wewe ni tatizo. Tuishi kwa kila mmoja kubeba madhaifu ya mwenzie kwa kuombana msamaha kwa yale yanayobebeka maana kuna mengine kuendelea kuyabeba ni kujitafutia ugonjwa wa moyo-**Aunt Ezekiel.**



## Banana Zorro atoa ya moyoni

KIONGOZI na mmiliki wa B-Band, Banana Zorro amesema yeye ni miongoni mwa wasanii wa mwanzo waliopata nafasi ya kujulikana na kupata umaarufu mkubwa kupitia kituo cha televisheni cha ITV.

"Huwezi kuzungumzia ITV bila kumtaja Mengi, bila yeye kuanzisha chombo hicho huenda nisingejulikana, kwani wimbo wangu wa kwanza wa 'Anakudanganya' ulitangazwa sana hadi nikajulikana. Kifo chake kimenigusa sana, alikuwa kioo cha mafanikio na mpenda maendeleo," amesema Banana.

Amesema historia ya Dk. Mengi ilionyesha kupitia changamoto nyingi bila kukata tamaa kufikia mafanikio makubwa na hakuwa mchoyo kusaidia wahitaji wa aina mbalimbali wakiwamo walemavu.

UNASEMAAA...

## Aunt Lulu: Tangulia Baba Mengi

MWIGIZAJI wa filamu Lulu Semagongo, 'Aunt Lulu' amewaomba Watanzania kuishi maisha ya kujishusha kama ilivyokuwa kwa Dk. Reginald Mengi kwa vile ndio njia mojawapo ya kumpendeza Mungu.

"Mzee wa watu alikuwa ni mtu wa kujishusha, hakujali utajiri alionao na badala yake alishuka hadi kuwafikia watu wa chini kabisa ndio maana kifo chake kimeumiza watu wengi," amesema Aunt Lulu.

Amesema yeye (Aunt Lulu), ameumia na amekumbuka jinsi Dk. Mengi alivyomwezesha kupata nafasi ya kutangaza kipindi cha Watoto Shoo cha kituo cha ITV na kupata jina kubwa kwenye jamii.

"Bila Mengi nani angenijua mimi Aunt Lulu? Kifo chake kimeacha pengo kubwa sana, ninaomba watoto wake wasimame imara kuendeleza makampuni yote ya IPP ili kumuenzi mzee wetu," amesema.






## Mgendi apata fundisho toka kwa Mengi

JENNIFER Mgendi amesema ni mara chache kupata watu wa aina ya Dk. Mengi ambao wanatumia utajiri wao kuwasaidia wanyonge ili nao wainuke.

Mwimbaji huyo wa nyimbo za Injili, amesema Dk. Mengi amesaidia wanyonge wengi na amejiwekea hazina yake mbinguni, na kufafanua kuwa hivyo ndivyo wacha Mungu huwa wanafanya.

"Alijali wanyonge kwa kutumia utajiri wake kuwafanya wajisikie ni wa thamani. Nitamkumbuka kwa uthubutu uliomwezesha kuwa na mafanikio makubwa kiuchumi...ametuachia mambo ya kujifunza," amesema Mgendi.

BODA 2 BODA



## Siboka akumbuka ushauri wa Mengi

MSANII wa nyimbo za asili, Costa Siboka, amesema atakumbuka ushauri wa Dk. Reginald Mengi wa kumtaka achague fani moja ili aweze kufanikiwa kwenye sanaa.

"Zamani nilikuwa mtunisha misuli, kisha nikageukia muziki wa asili nikawa ninafanya vyote kwa pamoja, lakini aliniambia nichague kimojawapo na kukiendeleza ndipo nikaacha utunishaji wa misuli," amesema Siboka.

Siboka amesema ushauri huo umesaidia kumfanya awe na mafanikio makubwa katika muziki wa asili kwa kupata maonyesho mengi nchini hali inayomwezesha kumudu maisha yake ya kila siku.

Mengi alikuwa mtu wa kujishusha na kuzungumza na watu wa kawaida kama mimi bila kujali utajiri wake. Hili linafaa kuigwa na matajiri wengine," amesema.




@burudanitele

**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



Poleni sana familia, dah inaumiza sana. Mbele yake nyuma yetu R.I.P Dk Reginald Mengi-**Tausi Mdegela.**



Asante kwa kila kitu R.I.P Mwenyekiti Dk. Reginald Mengi-**Lady Jaydee.**



Mungu akupe pumziko la milele Dk Reginald Mengi. Asante kwa upendo wako na kuthamini wanyonge. Namshukuru Mungu kwaajili yako. Mimi naitwa Happiness ila nimekua Nyamayao kupitia ITV ambayo ni mali yako, ambayo wewe uliruhusu tuweze kuonesha vipaji wakati huo wengine walichukulia sanaa kama uhuni . Mwendo umeumaliza, pumzika kwa amani-**Nyamayao.**

1.
2.
3.
4.
5.

# Kuumbe!



## BURIANI BERESA KAKERE

# Mwanamuziki aliyeibwa usiku na Msondo

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara nyingine tena, tasnia ya muziki wa dansi imekumbwa na msiba mkubwa baada ya kuondokewa na mwanamuziki mkongwe nchini Beresa Kakere.

Huyu ni mdogo wa marehemu Juma Kakere, ambaye pia ni mwanamuziki nguli na ndiye aliyethibitisha kifo cha kaka yake. Amesema alifariki asubuhi Jumatano iliyopita nyumbani kwake, Barabara ya Nne Jijini Tanga.

"Baada ya kuona anachelewa kuamka, majirani zake wakamgongea mlango bila mafanikio, wakaamua kuvunja na kumkuta amefariki dunia, " alisema Juma, ambaye ni mtunzi wa nyimbo za muziki wa dansi 'Betty' na 'Safari' zilizotamba mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Juma alisema kuwa kaka yake alikutwana mauti, akiwa hana jeraha lolote na wiki mbili zilizopita alikuwa naye. Hivyo anaamini, ni kifo cha ghafla. Beresa alizikwa siku hiyo hiyo ya Jumatano jioni mjini Tanga na kwa mujibu wa mdogo wake Juma, hajaacha mke wala mtoto.

Beresa Kakere ni nani?

Huyu anaingia katika orodha ya wanamuziki wa dansi wenye vipaji vya hali ya juu kuwahi kutokea nchini.

Ni mzaliwa wa jiijini Tanga na kusoma Shule ya Sekondari Karimjee mwaka 1969, huku mambo ya muziki akijifunza kutoka kwa nguli wa muziki marehemu John Kijiko kwenye bendi ya Jamhuri Jazz ya mjini Tanga.

Baadaye alikwenda nchini Kenya na kupiga muziki kwenye miji ya Nairobi na Mombasa, kabla ya kurejea nchini mwaka 1976, hapo alijiunga na bendi ya Biashara Jazz Band 'Wana 'Dunda Dunda', ambayo kwa wakati huo ilikuwa juu katika anga za muziki wa dansi nchini.

Huko, mara moja alionyesha umachachari wake, kuwa si nyota wa kubabaisha, alipotunga kibao maarufu cha 'Clara', ambacho kinaendeleza uenyeji wa kutamba katika albamu za muziki wa dansi nchini.

**Alivaa viatu vya Majirani Dar International**

Mnamo Januari mwaka 1978 aliingia studio za RTD akiwa na bendi mpya ya Dar International na kurekodi kibao kilichompatia umaarufu zaidi kiitwacho 'Magrareth'. Kipande cha kutuma kwenye wimbo huo, awali kilikuwa kikiimbwa na Marijani Rajab, lakini baada ya kutimuliwa kwenye bendi hiyo na kiongozi wa kwanza wa bendi hiyo Abel Bathazar, ndipo Kakere alipopewa akimbishe.

Kwa kweli alikitendea haki, kiasi cha bendi kubwa nchini kuanza kummezea mate. Ikumbukwe kuwa Marijani alirejea tena kwenye bendi hiyo, baada kina Bathazar kwenda kuunda Mlimani Park Orchestra mwishoni mwa mwaka huo wa 1978, kilichokuwa na makazi yake kwenye ukumbi wa Mlimani Park, jirani na Mlimani City jijini Dar es Salaam.

**Kakere alivyotekwa na Msondo**

Wakati asilimia 90 ya wanamuziki wa Dar International wakienda kuunda Mlimani Park Orchestra, kuna baadhi ya wanamuziki walibaki na kuungana na Majirani kuendeleza bendi, lakini Kakere na swahiba wake mcharazaji wa gitaa la solo, Kassim Mponda walitimkia Vijana Jazz Band, ambayo waliifanyia kazi kwa siku moja tu.

Wakiwa katikati ya shoo kwenye Ukumbi wa DDC Kariakoo, kuna watu waliingia na kuwatonya kuwa wanaitwa mlangoni.

Huko walikutana na ujumbe wa watu waliokuja na gari aina Land Rover 109 la Juwata na kuambiwa wanahitajika na bendi hiyo iliyokuwa na onyesho DDC Magomeni Kondoa.

Kakere na Mponda hawakujivunga, kwa sababu Juwata Jazz Band wana Msondo Ngoma ni bendi kubwa mno nchini, hivyo wakaingia kwenye gari na kuelekea huko na moja kwa moja wakaajiriwa kama wanamuziki rasmi.

**Wimbo wake ulikataliwa na kuwabeba Msondo**

Katika maisha yake mapya huko Msondo Ngoma, tayari Kakere alikuwa na wimbo aliotoka nao Vijana Jazz Band uitwao 'Sogea Karibu'. Kwa sababu ndiyo kwanza alikuwa ameingia na ukapangiliwa uingie katika orodha ya nyimbo za kurekodiwa RTD.

Kama inavyojulikana, hulka za baadhi ya wanamuziki kuwa na 'nyodo' nako Msondo Kakere alikutana nao. Hao waliongozwa na wapiga ala za upepo waliousua, lakini wanamuziki wachache wakiongozwa na mwimbaji Hassan Rehani Bitchuka na mpiga kinanda Waziri Ally, ndiyo waliokomaa kuwa 'ni lazima ukamilike.'

Ajabu ni kwamba, ndiyo wimbo uliotokea kupendwa mno kwenye kumbi na kuwafanya wanamuziki kutuzwa pesa nyingi, kiasi cha wale waliousua kutaka kupanda stejini ili kuingiza vionjo, ili nao waambulie vijisenti, lakini walikuwa wakikataliwa na wenzao waliokomaa mazoezini hadi ukakaa sawa na kurekodiwa kwa vionjo vitamu maradufu.

Wimbo huo ukawa maarufu mno mwaka 1979, uliporekodiwa na huenda ukawa ndiyo wimbo pekee wa Msondo, ambao haukupigwa ala za upepo, badala yake kinanda cha Waziri ambaye kwa sasa yupo bendi ya Njenje, ndicho kilichotamba.

Nyimbo nyingine alizotunga akiwa na Msondo ni 'Utu ni Tabia Njema' na 'Nimekubali Makosa'.

**Alipotua Bima Lee**

Hata hivyo, baadaye aliondoka Msondo na kujiunga na bendi ya Bima Lee, ambako nako alifanya makubwa, hasa alipotunga nyimbo zilizokuwa maarufu mno wakati huo.

Hapo zinaingia katika orodha nyimbo hizo ni 'Asia', 'Ombi', 'Remmy', lakini kuna wimbo ambao ulitokea kuwa msamiati mitaani unaoitwa 'Chande' ambao ulikuwa na simulizi ya kinidhamu.

Uliibua msemo 'unasemasema ovyo kama Chande.' Kakere aliachana na muziki mwaka 1982, lakini baada ya miaka mingi, alirejea tena na bendi yake aliyoiita Djakabe Group na kutoa vibao kadhaa vilivyotamba, kabla ya kustaafu rasmi na masuala ya muziki, akihamishia uso wake kwenye biashara hadi umauti ulipomkuta.



# Wasanii wa 5 waliofuata nyayo za baba zao



**Na Adam Fungamwango**

MAJI hufuata mkondo wake. Mtoto wa nyoka ni nyoka. Hiyo ni misemo ya kiswahili inayoonyesha kuwa mara nyingi watoto hufuata tabia au mambo ambayo wazazi wao wanayafanya.

Ingawa si mara nyingi, au lazima iwe hivyo, lakini wanayoyafanya baadhi ya watoto wanaakisi kile ambacho wazazi wao wanakifanya.

Ndiyo maana unaweza kuona baba ni mcheza soka na mtoto anakuja kuwa hivyo hivyo, labda tofauti ndogo inaweza kuwa baba hakuwa staa, lakini mtoto akawa hivyo, au baba akawa maarufu, lakini mtoto akaishia mchangani.

Kuna wakati wote wanaweza wakawa mastaa kila mtu na wakati wake.

Leo tunawaangazia wasanii wa muziki wa kizazi cha sasa ambao wamerithi vipaji kutoka kwa baba zao.

Yaani baba zao walikuwa wanamuziki huko nyuma na baadaye watoto wao nao wakaja kuwa kama wao.

**Papy Kocha 'Mtoto wa Mfalme'**

Ni mwanamuziki ambaye anajulikana sana na kizazi cha sasa na cha kati. Mwanzoni mwa miaka ya 2000, aliwika akiwa na bendi za FM Academia, TOT Plus na Achigo Band.

Alifungwa jela mwaka 2004, kabla ya kutolewa kwa msamaha wa Rais Dk. John Magufuli mwaka 2017.

Kwa sasa bado anaendelea na muziki.

Papy Kocha yeye amerithi kazi ya baba yake Nguza Mbangu 'Viking', aliyekuwa kiongozi wa bendi ya Maquiz Du Zaire kwenye miaka ya '70 hadi mwanzoni mwa miaka ya '90.

Nguza ambaye kwa sasa anajulikana sana kwa jina la 'Babu Seya', aliwahi pia kupigia bendi ya Sambulumaa na kuanzisha bendi yake ya Achigo kabla kufungwa jela na watoto wake akiwamo Papy Kocha 2004 na kusamehewa 2017. Hata baada ya kutoka kifungoni, wote Baba na Mwana wanaendelea na mambo ya muziki.

Wakati Papy Kocha aliimba, baba yake ni mpiga gitaa la solo, besi na kuimba pia.

**Tx Moshi 'Junior'**



Huyu ni mtoto wa mwanamuziki wa zamani wa bendi ya Msondo Music, Tx Moshi William. Anaitwa Tx Moshi 'Junior', lakini jina lake halisi ni Hassan Moshi.

Kwa sasa ni mwanamuziki wa bendi aliyokuwa akipigia baba yake. Tx Moshi 'Junior', ni msanii mwenye vipaji vingi kwani kabla ya kurithi kazi ya baba yake aliwahi kujiingiza kwenye tasnia ya kuigiza na kucheza filamu kadhaa, kiasi cha kumfanya hata baba yake naye acheze baadhi ya filamu.

Mtoto wa Moshi, alijiingiza rasmi kwenye muziki wa dansi baada ya kifo cha baba yake mwaka 2006.

Kwenye bendi ya Msondo, Tx Junior ni mwimbaji kama alivyokuwa baba yake.

**Banana Zorro**



Banana Zorro ni mmoja wa wasanii nyota kabisa wa kizazi kipya kwenye muziki wa bongo fleva. Sidhani kama kuna kijana wa kizazi cha sasa hamjui. Ametunga na kuimba nyimbo nyingi sana maarufu ambazo zinapendwa na zitaendelea kupendwa. Huyu pia amerithi kazi ya baba yake.

Ni mtoto wa mwanamuziki iliyokuwa bendi ya JKT Mafinga, maarufu kama 'Kimulimuli' iliyokuwa na maskani yake mjini Iringa, Zahir Ally Zorro.

Baadaye mzee huyo alijiunga na bendi ya Sambulumaa na kutunga kibao kilichopendwa na wengi 'Cleopatra'.

Hadi leo Zahir anaendelea na shughuli za muziki kama mwanaye. Wote wana uwezo wa kupiga gitaa na kuimba.

**Kassim Mganga**



Anajulikana kama msanii wa bongo fleva, lakini kwa siku za karibuni amekuwa akiimba nyimbo zenye vionjo ya Pwani. Nyimbo zake za sasa nyingi anazifanya kwa mtindo wa mduara hivi.

Huyu pia amerithi kipaji hicho si kutoka kwa baba yake, tu bali pia mama yake.

Baba yake ni Hemed Mganga, aliyekuwa mwanamuziki aliyepigia bendi mbalimbali kama Atomic Jazz, Urafiki Jazz, UDA Jazz, Orchestra Makassy na Legho Stars, huku mama yake akiwa ni mwimbaji mwenye vikundi vya taarab Tanga, vikiwemo Bandari Modern Taarab na Coast Modern Taarab.

Mzee Hemed alikuwa ni mpiga gitaa la kati 'rhythm', huku mtoto wake Kassim yeye ni mwimbaji.

**Ochu Sheggy**



Naye pia ni mmoja wa wasanii wa kizazi kipya ambaye amerithi kazi kutoka kwa baba yake.

Ochu, ni mtoto wa mwanamziki wa zamani wa bendi za Super Rainbow, Vijana Jazz, Washirika Tanzania Stars na Bantu Group, Eddy Sheggy.

# Vijimambo

1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
22. Watu wa kizazi hiki, kweli wamedata. Haya bhana na selfii yako bandia - Mama Nah, Manzese DSM.
23. Kweli ushamba zigo la miba. Tangulini simu hiyo ikatumika kwa selifii? - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
24. Hiyo ni sawa na kuosha mchele kwenye mto wa maji mengi. Utapata taabu sana - Semeni Mpanjira, Kilwa.

**SMS Bomba ya Leo:**
Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**




# Ugomvi wa wazazi, mateso kwa watoto

**Na Adam Fungamwango**

WAGOMBANAPO mafahari wawili ziumiazo ni nyasi. Huu ni msemo wa Kiswahili wenye maana kuwa wanapogombana watu wenye uwezo unaofanana, basi wale walio chini yao ndiyo watakaoathirika.

Mtunzi wa filamu ya 'Denti' amejaribu kuliangalia hili ndani ya jamii na kuja na kitu kama hiki kwa ajili ya kuelimisha.

Mara nyingi wanapogombana wazazi, wao hawaathiriki sana na ugomvi huo kwa sababu kila mmoja ana mtazamo wake au malengo yale, lakini watoto ambao wanawategemea baba na mama kuwa kitu kimoja, kukaa pamoja na kuwalea ndiyo wanaoteseka na athari za zao huonekana mapema zaidi kuliko hata za wanaogombana wenyewe.

Waliocheza filamu hii ni Blandina Chagula aliyecheza kama mke wa Deo, Slim Omari ambaye ndiye Deo mwenyewe, Gladyness Steve aliyecheza kama Linda, Afsa Omari Thageo Alexander na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha kuwa Deo na mkewe wakigombana kiasi cha kupigana. Binti yao Linda anashuhudia ndondi hizo, lakini anaonekana kuumizwa mno na tabia ya wazazi wake ambao kila kukicha wao ni kubishana, ugomvi na ngumi.

Mawazo kichwani wanamfanya hadi kutofanya vema darasani. Walimu wanashangaa kwani awali alikuwa denti mwenye akili nyingi.

Linda analieleza tatizo la wazazi wake kwa rafiki yake wa jirani. Hakuna rafiki mwema, kwani anamshauri kujisahahulisha mambo hayo kwa kunywa pombe, na anasa. Anakataa kufanya hivyo. Lakini kila kukicha ni afadhali ya jana. Mwisho anaamua kuungana na rafiki yake. Linda anabadilika tabia. Anaanza kunywa pombe, kufuta sigara na kufanya ngono zembe.

Siku moja mama yake anaondoka na kurudi usiku wa manane na kuomba afunguliwe mlango. Mumewe Deo anakataa na kumwambia akalale huko huko alikotoka. Anampiga marufuku Linda kwenda kumfungulia mama yake.

Hali inazidi kumchanganya Linda, ikawa ni tabia yake akitoka shuleni anapitia kwa wanaume zake kwa ajili tu ya kuondoa msongo wa mawazo kwa sababu ya matatizo ya nyumbani kwao.

Siku moja anaamua kwenda anakokutana na rafiki zake, lakini hawakuti. Anajaribu kwenda kijiwe kingine anakutana na mvulana anayemtongoza ili kufanya naye mapenzi. Akakubali, lakini wakati wanaingia chumbani tu, anakutana na wavulana wengine wawili ambao wote wanambaka.

Hali hiyo inazidi kumchanganya Linda na anaamua kutokwenda kabisa shule. Kama kawaida wazazi wa Linda wanaanza kugombana kutokana na kubadilika kwa tabia ya binti yao kila mmoja akimtuhumu mwenzake.

Walimu wake wanaamua kumsaka kwa sababu hafiki shule na nyumbani hakai sana. Wanamfuma kwa mpenzi wake akiwa hajiwezi kwa kutumia madawa ya kulevya.

Walimu anamchukua na kumpeleka hospitalini ili apate matibabu. Wanawasiliana na wazazi wake, lakini wanapokutana hospitalini kazi ni ile ile tu, ugomvi.

Walimu wanawaamua na kuwakalisha chini wakiwaambia kuwa ili kuokoa maisha ya mtoto wao, asiendelee na tabia aliyonayo, ni wao kuyamaliza yote na kuishi kwa amani nyumbani, vinginevyo wanampoteza mtoto wao. Wakaahidi kubadilika tabia mbele ya walimu wa binti yao.



# KWAHERI MOSESENGO FAN FAN, RAFIKI WA FRANCO

**Na Adam Fungamwango**

MASHABIKI wa muziki wa dansi Afrika Mashariki na Kati walipatwa na mshtuko, baada ya kutangazwa kifo cha mpiga gitaa la solo maarufu, Mosesengo Fan Fan Mei 3 mwaka huu.

Taarifa zikasema kuwa mwanamuziki huyo mkongwe alifariki dunia nchini Kenya, baada ya kuanguka ghafla kwenye eneo alilokuwa anaishi Thika Super Highway na kukimbizwa kwenye Hospitali ya Kasarani, lakini baada ya vipimo ikaonekana kuwa alikuwa ameshafariki dunia.

Alifariki dunia ikiwa ni siku mbili tu kabla ya kuzikwa mwanamuziki mwingine mkongwe waliokuwa kwenye bendi moja ya TP OK Jazz iliyokuwa ikiongozwa na Lwambo Luanzo Makiadi Franco, Lutumba Simaro ambaye alizikwa Mei 5 mjini Kinshasa.

Taarifa za awali zinasema kuwa kifo cha Mosesengo Fan Fan kilitokana na ugonjwa wa moyo.

Mwanamuziki huyo ambaye alikuwa akiishi London nchini England, alikwenda Nairobi nchini Kenya kurekodi baadhi ya vibao vyake pamoja na wanamuziki kadhaa wa hapo, akiwemo Paddy Makani na Disco Longwa.

Mosese ambaye alikuwa akipenda mno kuzuru Kenya mara kwa mara akitokea alikoweka makazi yake London, na mara ya mwisho 2016 alirekodi kibao kiitwacho 'Papa Fololo' ambacho kimeendelea kupendwa hadi leo nchini humo na wengi hasa kizazi cha sasa wameonekana kusikitishwa na kifo hicho, kutokana na kuupenda sana wimbo huo.

**Mwanamuziki wa TP OK Jazz**

Alizaliwa Oktoba 16, 1945 nchini Congo DR na kupigia makundi kadhaa nchini humo, zikiwemo bendi za Lovy Du Zaire chini ya Vicky Longomba, lakini bendi iliyomtambulisha zaidi na kumpa sifa ni TP OK Jazz chini ya Franco.

Mosese alikuwa ni mpiga solo namba mbili baada ya Franco. Kabla Fanco hajawasili, au amechoka na kutaka kupumzika, mtu pekee aliyemuamini kumuachia gitaa ni Mosesengo tu, ndiyo maana hata upigaji wao ukawa unafanana, wote wakipiga kwa staili ya 'Kente' iliyoasisiwa na Franco mwenyewe.

Alitunga kibao kilipompatia sifa yeye na bendi nzima kiitwacho 'Dje Melasi' mwaka 1973.

Hayati Mosese na Yollou Mabiala walijiengua TP OK Jazz na kwenda kuunda kundi la Somo Somo lililofanya ziara mbalimbali kwenye nchi za Zambia na Kenya katikati ya miaka ya '70.

**Alikaa Bongo kwa miaka mitano**

Mwaka 1975 aliingia nchini Tanzania akiletwa na Mzee Makassy ambapo alifanya kazi kubwa kwa kupiga gitaa na kutunga nyimbo kadhaa kama 'Mosese', 'Nitakufa Bila Kisa', 'Molema', 'Cisca', na nyinginezo akiwa na Makassy, akipiga solo kwa kiwango cha juu na yoyote anayesikia anaweza kudhani ni Franco.

Mwishoni mwa miaka hiyo alikuwa mmoja wa waasisi wa Super Matimila na pia huko alipiga solo kwenye nyimbo kadhaa ukiwemo 'Bishada' uliotungwa na Skassy Kasambula.

Aliondoka nchini na kwenda Congo, lakini mwaka 1990 alirejea kwenye bendi yake ya zamani, lakini wakati huo sasa ikiitwa Bana OK, baada ya kifo cha Franco.

**Safari ya kwenda London**

Akiwa na baadhi ya wanamuziki wa Congo, Fan Fan aliamua kuondoka nchini kwao na kwenda London kuweka makazi, lakini akirejesha kundi lake la Somo Somo ambalo lilikuwa likitoa mara kwa mara albamu, lakini iliyovuma sana ni ile ya 'Hello Hello' aliyoitoa mwaka 1995, na hasa wimbo uliobeba jina la albamu ambao ulilipaisha zaidi kundi hilo, akiwa pamoja na kina Yollou Mabiala, Cyrian Mbenza, Dally Kimoko, Ballou Canta, Nyboma Mwandido na wengineo.

# VIJANA WA KUFOKAFOKA WANAOSHIKA CHATI DUNIANI



Ariana Grande



Alecia Beth Moore 'Pink,' anatamba kwa muziki wa Pop.



Lii Nas X



Billie Eilish



## Mionzi ya Sheria

Na John Juma
0716217615

# Darasa kamili Shauri la Mirathi linavyoendeshwa

KUNA masuala muhimu kufahamu, kabla ya kufungua Shauri la Mirathi katika Mahakamani za Mwanzo.

Ni mara nyingi, hususan kwa marehemu Wakristo, kushuhudia warithi, ndugu, au hata jamaa zake wanafungua Shauri la Mirathi Mahakama za Mwanzo. Jambo/hatua hiyo ni kinyume kabisa na matakwa/matarajio ya Sheria husika.

Na hii, kwa namna yoyote ile, haiathiriwi na ukweli kuwa marehemu kabla ya kufariki aliacha wosia(Testate); na hakuacha wosia(Intestate).

Madhali tu alikuwa ni Mkristo Mahakama ya Mwanzo siyo mahali sahihi, (pake).

**Maana/Tafsiri ya Mahakama za Mwanzo**

Mahakama za Mwanzo, zenyewe ziko kwa mujibu wa Sheria ya Mahakama za Mahakimu, 1984 (The Magistrates Courts Act Cap. 11) kupitiaKifunguchake cha 3(1)-(2).

Mara zote, katika maeneo zinakopatikana (mjini na vijijini ngazi za wilaya) ni rahisi kutambulika, kwani mbele yake huwekwa bango (kubwa au la wastani) lenye maneno yanayosomeka "MAHAKAMA YA MWANZO YA.........."

Ni zipi (hasa)Sheria husika?

Katika Masuala ya Mirathi, mahakama hujiongoza kwa kutumia/kuzingatia sheria za aina mbili (2), yaani zile za Kiutaratibu (Procedures Laws) na zile zinazoelekeza namna Mgawanyo wa Mali unatakiwa kufanyika (Substantive laws). Kwa kuzingatia haki/stahiki ya kila mhusika.

Isitoshe, hizo ambazo zinazoelekeza nani a pate nini na zenyewe zimegawanyika katika makundi/aina kuu tatu (3).

Hivyo basi, kila moja (kati ya hizo tatu) inasimamia kikamilifu kundi lake. Kundi linalosimamiwa na Sheria moja haliwezi kutumia Sheria ya kundi lingine. Kwani, zenyewe ziko tofauti kabisa, hali ya kuwa zinasimamia wajibu mmoja.

Moja, ni ile Sheria ya Mirathi ya India ya Mwaka 1865 (The Indian Succession Act); pili ni sheria iitwayo Sheria za Kimila [The Local Customary Law (Declaration) Order No. 4, 1963]; na ya tatu ni Sheria ya Kiislam (The Islamic law),ambayo kimsingi ni Qur-an na Hadith/Sunnah.

Ya kwanza, ni maalum kwa ajili ya Wakristo, wakati hiyo ya upili (yenyewe) ni maalum kwa Watu Wanaoishi kwa mujibu wa Taratibu za Kimila, ambao siyo Waislamu wala Wakristo; na ya tatu, hutumika (maalum) kwa ajili ya Waislamu.

Kile kinachoonekana hapa, mhusika anatakiwa/anatarajiwa kuandaa mirathi yake kutokana/kulingana na mtindo wake wa maisha. Na siyo kinyume na Sheria inavyomtaka.

**Mambo Muhimu**

Mirathi huanza kutambulika rasmi tangu (siku ya kwanza) mhusika anapoandaa wosia wake (vile angependa mali zake zigawanywe/kutumikia mara baada ya umauti kumfika) na kuishia pale usimamizi au mali za marehemu zinapokwisha kugawanywa kwa warithi wake.

Jukumu ambalo linatekelezwa na Msimamizi mkuu wa Mirathi husika mara baada ya kuthibitishwa na Mahakama. Kifungu cha 2(1) na kipengele cha VIII, Sheria ya Mirathi Suraya 352.

Nyongeza, Sheria za Kiutaratibu (Procedures laws) ni kama, Sheria ya Mahakama za Mahakimu, 1984 (The Magistrates Courts Act Cap. 11) na Sheria ya Mirathi Sura ya 352,(PAEA).

Kwanini siyo sahihi Wakristo kufungua Mirathi katika Mahakama husika?

Kwa kujibu wa Jedwali la 15, kipengele cha 1(i) cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu, 1984 (The Magistrates Courts Act, Cap. 11) kinaelekeza, Mahakama ya Mwanzo, yenyewe, itakuwa na mamlaka katika masuala ya mirathi iwapo sheria husika inayotumika katika mirathi, ni ama Sheria ya Kiislamu (The Islamic law) au Sheria za Kimila [The Local Customary Law (Declaration) Order No. 4, 1963].

Hii ni sawa na kusema, (kwa mujibu wa awali), Mahakama ya Mwanzo itatumika endapo tu marehemu alikuwa Muislamu au aliishi maisha yake kimila.

Hivyo basi, Mahakama inayotumika (nchini) kwa ajili ya Usimamizi wa Mirathi ya Marehemu Wakristo ni Mahakama Kasimu ya Wilaya (District Delegate), kwa mujibu wa kifungu cha Tano cha Sheria ya Mirathi Sura ya 352. Yenyewe, (Mahakama Kasimu ya Wilaya), inapatikana popote ilipo Mahakama ya Wilaya ya Kawaida.

**Hitimisho**

Mathalani, makundi yote hayo (Waislamu, Wakristo na Watu wa Mila) bado sheria husika zinaruhusu (wao) kuitumia Mahakama Kuu kwa shughuli za mirathi kwa mujibu wa Kifungu cha Tatu cha Sheria ya Mirathi, Sura ya 352, kwa kuwa ina mamlaka ya jumla, sanjari na Kifungu cha18 (1)(a) (i), Sheria ya Mahakama za Mahakimu, 1984 (The Magistrates Courts Act Cap. 11).

Naomba kuwasilisha.



## Kalamu ya Mwalimu

Reubeni Lumbagala

# Vijana wabunifu aina hii waendelezwe kiteknolojia

KAMA kuna Mtanzania anadhani nchi yetu haina vijana wenye uwezo wa kufanya mambo makubwa ya kushangaza dunia, hasa katika nyanja ya sayansi na teknolojia, basi atakuwa anakosea sana.

Tanzania imejaliwa kuwa na vijana wengi wabunifu ambao kama wakitumiwa ipasavyo, nchi yetu itapiga hatua kubwa katika maendeleo ya sayansi na teknolojia na hatimaye mipango ya serikali ya kuifanya nchi kuwa ya Viwanda na Uchumi wa Kati, ifikapo mwaka 2025 kufanikiwa kwa urahisi kabisa.

Ubunifu ni nyenzo muhimu katika maendeleo ya sayansi na teknolojia na ndiyo maana, serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), wanatoa mkazo kwa wanafunzi wengi kusoma sayansi, ili kutumia maarifa yao ya sayansi na teknolojia katika kusaidia maendeleo ya nchi yetu.

Wanafunzi wakiyatumia vizuri maarifa wanayoyapata katika masomo yao ya sayansi, pamoja na vipaji walivyojaliwa na Mwenyezi Mungu, wana uwezo wa kubuni na kutengeneza vitu vikubwa, kama mashine na mitambo, ambavyo vinahitajika katika kurahisisha utendaji kazi wa kimaendeleo.

Gabriel Jeremiah, ni mhitimu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kilichopo jijini Dar es Salaam, katika Shahada ya Uhandisi Mitambo (Bachelor of Mechanical Engineering).

Jeremiah, amefanikiwa kutengeneza gari linalotumia mfumo wa umeme wa betri, badala ya mafuta kama ilivyozoeleka kwa watu wengi.

Gabriel anasema, gari hilo likijaa vizuri chaji, lina uwezo wa kusafiri umbali wa kilometa 90. Gari hilo limefungwa mota ambazo zinatumika katika kusukuma magurudumu ya gari.

Kasi ya magurudumu ya gari, inategemeana na nguvu ya umeme inayosukuma mota iliyofungwa. Kwa mujibu wa Gabriel, gari lina uwezo wa kwenda kasi ya kilometa 80 kwa saa. Kijana Gabriel alishirikiana kwa karibu na mwanafunzi mwenziwe anayemtaka kwa jina la Mtatiro Boniface.

Gabriel anasema gharama za kuchaji gari hilo, ili liweze kusafiri umbali wa kilometa 90, ni umeme 'units' tatu kama unaotumika majumbani kwa gharama ya Sh. 1200 za Kitanzania.

Vijana hao wanaendelea na kazi yao ya kurahisisha usafiri huo na wapo katika mkakati wa kulifanya gari hilo liweze kujichaji lenyewe, pindi linapoendeshwa, ili liwe na uwezo wa kusafiri umbali mrefu zaidi.

Ubunifu uliofanywa na vijana hao, ni kielelezo kuwa kama elimu yetu itatilia mkazo kwa vitendo, kuliko nadharia, wanafunzi wa Tanzania watafanya mambo makubwa na ya kushangaza ulimwengu.

Wakati umepita kwa wanafunzi kukaririshwa nadharia za masomo, bila ya kuingiza katika vitendo, kwani kuendeleza elimu ya nadharia zaidi, matokeo yake hayatafika mbali.

Nchi yetu itashindwa kupata wabunifu, wataalamu walioiva vizuri katika fani mbalimbali, wanasayansi na wataalam wa teknolojia ambao ni nguzo muhimu katika maendeleo ya nchi yeyote ulimwenguni.

Ubunifu huu umeonyesha umuhimu wa tafiti katika kukuza maendeleo ya nyanja mbalimbali za kimaendeleo. Kabla ya kukamilika gari hilo, walifanya utafiti wa uwezekano wa kutengeneza gari linalotumia umeme wa betri badala ya mafuta.

Ni utafiti ulioonyesha suala hilo linawezekana na ndiyo maana vijana wakaingia kazini kutekeleza mpango huo ambao walitumia miezi mitatu, kuandika na miezi mitatu kukamilisha utengenezaji wa gari hilo.

Hivyo, serikali inapaswa itenge bajeti ya kutosha katika kutekeleza utafiti katika vyuo, taasisi na wizara mbalimbali, ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo.

Ubunifu wa vijana hawa umeonyesha pia umuhimu wa kutiana moyo, pale mwingine anapoonyesha nia ya uthubutu katika jambo fulani la kimaendeleo.

Kijana Gabriel anasema, aliliwasilisha wazo lake la kutengeneza gari linalotumia umeme kwa mwalimu wake ambaye baada ya kusoma andiko hilo la namna ya kutekeleza mradi huo, alimpongeza na kumhakikishia chuo kitafadhili gharama za utengenezaji gari hilo.

Kama Gabriel angekatishwa tamaa na mwalimu wake au na wanafunzi wenzake pindi alipowasilisha wazo lake la kutengeneza gari kwa njia ya maandishi, pengine angevunjika moyo na kughairi kutengeneza gari hilo, ambalo limethibitisha azma ya ubunifu huo.

Watanzania tunaweza kufanya mambo makubwa katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia.

Jambo jingine muhimu la kujifunza kupitia vijana hawa, ni kuwa bila uthubutu ni vigumu kufanikiwa. Gabriel alitanguliza uthubutu na kuamini kuwa anao uwezo wa kutengeneza gari linalotumia umeme.

Akauweka uthubutu huo katika vitendo na ndipo azma yake hiyo ilipotimia na kufanikisha kutengeneza gari. Ni lazima vijana wa Kitanzania wakawa na uthubutu na kuamini wanaweza.

Hata itakapotokea Mtanzania anavunjwa moyo na wale wanaomzunguka katika kile anachopanga kufanya, azibe masikio na kuamini inawezekana kukamilisha ndoto alizonazo kuwa uhalisia.

Serikali na wadau wengine wote wanapaswa kuwa tayari kuwasaidia vijana wenye uthubutu, kama hawa kwa maslahi mapana ya nchi yetu. Tafakari

• **Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Taaluma wa Shule ya Sekondari Mlali, iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Simu yake: (+255) 0764 666349.**

# Mnyama Duma katika hatua z



Duma akiwa katika mawindo yake katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

## ■Wako 9%; nchini
## ■Soko kuu la mag
## ■Ana mbio za gari



Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori nchini (TAWIRI), Dk.Simon Mduma.

**Novatus Makunga,** ARUSHA

WAKATi Wanasayansi watafiti wa maeneo mbalimbali duniani wanatahadharisha tishio la kutoweka mnyama Duma, kutokana na sababu mbalimbali. Lakini, Tanzania bado ina nafasi kubwa ya kuwatumia wanyamapori hao wenye kasi zaidi, kama kivutio cha utalii. Hiyo ni kutokana na idadi nzuri waliopo.

Duma ni kati ya wanyamapori 10 adimu aina za paka. Hadi sasa inaelezwa ni asilimia tisa tu ya aina hiyo ndio wamebakia duniani. Wengine wanaofanana nao Chui na Chui Milia

**KASI YAO**

Mnyama huyo ana mwendokasi wa kati ya kilometa 105 na 130 kwa saa na kwamba ana uwezo wa kuchanganya kasi hiyo kwa muda mfupi, mara tu anapoanza kutimua mbio.

Wanasayansi watafiti kutoka nchi mbalimbali. wamekuwa wakitahadharisha kwamba idadi ya duma duniani imepungua na kwamba kwa sasa jumla yao hawazidi 7,100.

Wanyama hao katika kipindi cha miaka 100 iliyopita walikuwa zaidi 200,000 duniani. Hiyo inayotokea, huku. Ni hivi karibuni, Umoja wa Mataifa ilitamka kwamba uharibifu wa mazingira, unahatarisha zaidi ya wanyama milioni moja kutoweka.

Mashirika yanayojihusisha na uhifadhi, yanasema kuwa wanyama hao wako hatarini kutoweka katika uso wa dunia, zikiwemo: Shirika la Utafiti wa Wanyamapori Nchini (TAWIRI); Shirika la Hifadhi za Taifa Nchini(TANAPA); Shirika la Kimataifa la Muungano wa Uhifadhi (IUCN); Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira na Wanyamapori (WWF); na Shirika la Wanyamapori Afrika(AWF)

Wanyamapori wanaoishi barani Asia, hivi sasa wanaathiriwa zaidi na idadi ya duma wanaoishi nchini Iran, ni chini ya 50 tu, lakini idadi ya duma wailoko nchini Zimbabwe, imepungua kuwa 170 kutoka 1200 katika miaka 16 iliyopita.

Naibu Mkuu wa Harakati ya Kuwalinda Duma Nchini Iran, Rajab Ali Karhar, anasema wahifadhi wa wanyamapori nchini humo, wameanza harakati za kuwalinda duma aina ya 'Asiatic', anayekabiliwa na hatari ya kutoweka katika uso wa dunia.

Meneja Mradi wa Mtandao wa Ufuatiliaji Biashara ya Wanyamapori, Traffic Washingiton DC nchini Marekan, William Crosmary, anasema awali wanyama hao walipatikana katika bonde la Mto Congo hadi Mashariki mwa India, lakini hivi sasa wanapatikana kwa asilimia tisa tu, katika sehemu za awali, hasa Kusini na Mashariki mwa Afrika.

**DUMA WA TANZANIA**

Meneja wa Mradi wa utafiti wa Duma nchini, Denis Minja, anaeleza hivi sasa ni asilimia 3.55 tu ya Duma waliobakia katika nchi mbalimbali duniani ni Tanzania, wako kati ya 700 na 800.

Kwa mujibu wa Tawiri, hivi sasa asilimia 90 ya duma wanapatikana barani Afrika na Namibia inaongoza kwa kuwa na Duma zaidi ya 2,000 wanaopatikana katika mashamba ya wakulima wakubwa.

Mtafiti Denis Minja, anasema katika mfumo wa Ikolojia ya Selous-Mikumi, Duma wametoweka tangu miaka ya 1980

Tofauti na nchi nyingine, mwendokasi wa magari katika hifadhi za taifa na baadaye kugongwa inatajwa kama moja ya sababu zinazochangia kupungua kwa Duma.

Takwimu za Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, zinaonyesha kati ya mwaka 2016 na 2018, Duma wapatao wanane walikufa, kutokana na kugongwa na magari ya watalii.

"Pamoja na adhabu kali, mfano aliyemgonga na kusababisha kifo cha Duma aliyekuwa anaitwa Rozi, alitozwa faini ya Dola za Marekani 5,000 (Sh. Milioni 11.5) na kuzuiwa kuingia katika mbuga kwa miezi mitatu lakini bado ajali hizi ni janga kubwa," anafafanua

**FISI, SIMBA, CHUI TISHIO**

Tishio lingine kubwa kwa duma ni wanyama Fisi, Simba na Chui kwa kula watoto wa Duma mara wanapozaliwa, kati ya Duma 100 wanaozaliwa ni asilimia tano, tu ndiyo wanaofanikiwa kuendelea kuishi.

Minja anaeleza kuwa mnyama Duma, ni miongoni mwa wazazi wazembe katika kulea na kutunza watoto, kwani huwaacha bila ya ulinzi katika eneo lao la makazi na wanaishia kushambuliwa na kuliwa na Simba ,Chui pia Fisi.

**BIASHARA HARAMU**

Watafiti wanasayansi, wanataja sababu nyingine inayopunguza idadi ya duma ni ujangili wa kuwawinda, kwa ajili ya biashara nje ya nchi husussani, katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) ambako ni kivutio kikubwa na huuzwa kati ya Dola za Marekani 5,000 (Sh. milioni 11.5) hadi dola 15,000 (Sh. Milioni 34.5).

Katika nchi za Kiarabu; Qatar, Kuwait, Bahrain na Saudi Arabia, Duma wanaowindwa na kukamatwa kutoka barani Afrika, wanatumiwa kinyume cha sheria kama wanyama wa kuishi nao.

Kwa mujibu wa watafiti wa wanyamapori, takribani Duma 300 wanawindwa misituni katika maeneo yao, na kupelekwa katika makazi ya binadamu mjini Riyadh au Abu Dhabi.

Takriban wanyama kati ya 1,200 hadi 1,500 walichukuliwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

"Takwimu hizi zinaweza kuonekana kuwa za kawaida, ikilinganishwa na ukweli wa mambo," anasema Crosmary.

Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO), yanakadiria kuwa zaidi ya nusu au hata theluthi mbili za wanyama hufa wakiwa njiani, kwa kukosa huduma ya afya.

Duma wanaohifadhiwa katika vyumba na wakati mwingine bafuni, hulishwa vyakula vya paka na wakati mwingine pipi au vyakula vyenye sukari, hupatwa na magonjwa haraka na mara nyingi hufa muda mfupi sana.

Mkurugenzi Msaidizi wa Mikakati, Mawasiliano na Mapambano ya Biashara ya Wanyamapori katika Shirika la Cheetah Conservation Fund (CCF) lenye makao makuu yake nchini Namibia na mwandishi wa taarifa nyingi kuhusu biashara ya duma, Patricia Tricorache mwezi Septemba mwaka jana, walitoa picha kwenye mitandao ya kijamii kuhusu mawindo na

# za mwisho kutoweka duniani

## wamebaki 700
## endo Uarabuni
## ' Km. 130 kwa saa





Duma aliyewekwa kwenye kasha maalumu, kwa ajili ya kusafirishwa na majangili kwenda nje ya nchi akiwa amekamatwa katika moja ya matukio yaliyotokea mjini Arusha. **PICHA ZOTE: NOVATUS MAKUNGA.**

ufugaji wa Duma na athari zake.

"Kati ya mwaka 2012 na 2017 nimehesabu Duma 1,367 wanaowindwa kwa ajili ya kuuzwa katika maeneo ya Ghuba, yaani, sawa na asilimia 20 ya Duma wanaoishi porini," alibainisha Tricorache.

Anasema, matangazo mengi yanatolewa kwenye mitandao ya kijamii hasa kutoka Saudi Arabia, ambako wafanyabiashara wanaingiza picha za video bila ya hofu, bei za duma wanaouzwa na namba zao za simu, mahali wanakopatikana na wakati mwingine kuna hata jina na picha ya aliyejipiga na mnyama huyo zinazojulikana kama 'selfie'.

"Majangili wana uwezo wa kuwakamata zaidi maeneo ya Kusini mwa Bara la Afrika. Idadi ya wanyama hawa inaweza kupungua miaka 15 ijayo, kulingana na hali inayoendelea na kwa kasi hii. Kuna uwezekano wa Duma kutoweka katikati ya karne hii," anaonya Tricorache.

Biashara ya duma, mnyama aliyeorodheshwa katika Kiambatisho Namba Moja cha Mkataba wa Washington kuhusu Biashara ya Wanyama walio Hatarini Kutoweka (CITES), ni marufuku.

### HATUA KUCHUKULIWA

Kuanzia mwaka 2015, japo uchukuaji hatua ulichelewa, lakini CITES ililipa kipaumbele suala ya ukomeshaji biashara ya Duma na tangu wakati huo, ilichukua mapendekezo mbalimbali na kuanza kuchapisha vipeperushi kama njia ya kutoa angalizo na mafunzo kwa maofisa wa forodhani, mipakani na viwanja vya ndege.

Kuna nchi za Ghuba zilizoimarisha sheria za kupiga marufuku biashara ya duma na zilianza kutumika mwaka 2017, katika nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Ni sheria inayozungumzia adhabu kwa wamiliki wa wanyama walio hatarini kutoweka, kwa kulipa faini kati ya Euro 2,300 hadi 167,000 na kifungo cha miezi sita gerezani.

"Duma siyo shida kwetu tena. Upatikanaji wao katika mitandao ya kijamii sasa ni mdogo na kwa wafanyabiashara kuwa na duma nyumbani siyo jambo la kawaida tena." anasema Ofisa Mwandamizi wa Mamlaka ya Mazingira ya Kuwait, Shereefa Al-Salem.

Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) nchini Somalia, yamejikusanya kupambana na biashara ya duma ambalo inadaiwa bandari kubwa ya nchi hiyo ya Berbera, ndiyo kitovu cha biashara yake.

Mtaalamu wa Shirika la Mfuko wa Duniani unaofadhili miradi ya mazingira, Colman O'Criodain, anaishutumu serikali ya Somalia, kwa kuitenga bajeti ya Wizara ya Mazingira ya Somalia inayokadiriwa kuwa Dola za Marekani 30,000 (Sh.milioni 69) akisema ni takribani sawa na bei ya Duma wadogo wawili.

Waziri wa Maendeleo na Mazingira nchini humo, Shukri Ismail Bandare, anasema mwaka jana majangili wawili walitiwa mbaroni na kisha walihukumiwa faini ya Dola 300 (Shilingi 690,000) na kutumikia kifungo cha miaka mitatu gerezani.

### UJENZI & KILIMO

Changamoto nyingine ya kupungua Duma, inatajwa ni kuwepo ongezeko la shughuli za kibinadamu hususani magari, ujenzi wa makazi na kilimo katika maeneo yaliyokuwa ni makazi ya Duma.

Watafiti kutoka Shirika la Wanyama la London, Shirika la Uhifadhi wa Wanyamapori wa Familia ya Paka la Panthera na Shirika la Uhifadhi wa Wanyama pori nchini Uingereza, walifanya utafiti na kutoa ripoti kwenye gazeti la Proceedings of the National Academy of Sciences la Marekani.

Walibainisha sababu za kupungua Duma, kuwa ni pamoja na kuvamiwa kwa makazi, kupungua chakula chao, kutokana na kasi ya uwindaji wa wanyamapori ambao ni chakula cha Duma, pamoja na uwindaji haramu na biashara haramu ya duma.

"Maeneo yao wanayoishi yamepungua kwa asilimia tisa na hali mbaya zaidi ya wao kupata chakula, hasa kutokana na kasi ya uwindaji wa wanyamapori," inaeleza ripoti hiyo ya kitafiti.

### TANAPA NA NCAA

Minja anashauri Shirika la Hifadhi za Taifa Nchini (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), wadhibiti wingi wa magari kama ilivyo katika Mbuga ya Maasai Mara iliyopo Kenya, ambako magari ya watalii kati ya saba na nane tu ndiyo yanayoruhusiwa kuingia kwa wakati mmoja.

"Magari ya watalii yanayoingia katika hifadhi za taifa kwa wakati mmoja ni mengi, hufikia hatua ya kuvunja taratibu na sheria, kwa kuchepuka na kuingia katika majani, kwa lengo la kuwasogelea wanyama," anasema.

Minja anafafanua kuwa, ingawa kiuchumi ni jambo zuri na kuwepo zaidi ya kampuni 300 za kusafirisha watalii, lakini hiyo inahitaji angalizo kutokana na athari kubwa katika masuala ya ikolojia na uhifadhi wa wanyamapori

Anaeleza, kuwa maeneo yote ambayo awali yalikuwa makazi ya Duma, hivi sasa yamejengwa kambi za kulala wageni na kusababisha duma kuyahama makazi yao ya asili

Katika maeneo hayo kumekuwepo na ongezeko kubwa la watu na kusababisha maeneo hayo kupoteza uoto wake wa asili na kuwa changamoto kwa Duma ambaye huishi katika eneo la kilomita za mraba 800.

Nchini Zimbabwe, kunaelezwa Duma wamepungua kutoka 1,200 hadi 170 katika kipindi cha miaka 16, kutokana na mabadiliko makubwa ya umiliki wa ardhi uliosababisha maeneo mengine ya hifadhi kuangukia katika mgawo wa matumizi ya kilimo.

Mkurugenzi Mkuu wa Tawiri, Dk Simon Mduma, anasisitiza umuhimu wa kuchukua hatua za makusudi kumlinda duma, kutokana na uadimu wake.

Dk. Mduma anaeleza kuwa, Tawiri inatarajia kuanza utafiti wa mnyama huyo katika mfumo wa ikolojia ya Hifadhi ya Taifa Ruaha, iliyopo mkoani Iringa na Hifadhi ya Taifa ya Taramgire, mkoani Manyara

Anasema Duma anapatika katika mbuga tambarare zenye majani mafupi, akifanana sana na Chui, lakini ana rangi ya manjano na mabaka meusi. Ni mnyama anayependa kula wanyama kama vile swala na wengine wadogo

■ **Mwandishi wa makala anapatikana kwa Barua pepe: makunganova@gmail.com au Simu: (+255) 0784682268**

# Ushirika Liwale 'yakuna kichwa' soko la korosho msimu huu

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Msingi cha Ushirika Umoja, ni miongoni mwa vyama zaidi ya 20 vya ushirika vilivyopo wilayani Liwale, mkoani Lindi, vinavyokusanya mazao ya wakulima, kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.

Huo ni mfumo wa kukusanya mazao katika ghala maalumu lililosajiliwa na serikali, kwa ajili ya kuyauza kwa bei ya ushindani. Korosho zilianza kuuzwa kwa mfumo huo tangu katika msimu wa mwaka 2007/2008.

Chama cha Umoja, kimekuwa kikitumia utaratibu huo kila msimu kimevuka malengo iliyojiwekea katika kila msimu, kwa kukusanya korosho nyingi kutoka kwa wanachama wake zaidi ya 1,000.

Katika msimu wa mwaka 2017/2018, Umoja iliweka lengo la kukusanya tani 3,000 za korosho, lakini kikavuka hadi tani 4,660, lakini msimu uliofuata hali ikawa tofauti. Kwanini?



Mwenyekiti wa Umoja Amcos, Hassan Mpako, akisoma taarifa ya chama hicho. Wengine ni viongozi wenzake.



Mkutano wa Umoja Amcos ukiendelea. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

**MWENYEKITI**

Mwenyekiti wa chama hicho, Hassan Mpako, anasema katika msimu uliopita 2018/2019, walijiwekea lengo kukusanya tani 4,825, lakini wakajikuta wanaambulia tani 2,813 tu. Hiyo iliwafanya wayumbe kiuchumi.

Mwenyekiti huyo anawaambia hayo wanachama wake kuwa, Umoja Amcos, hivi karibuni kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa chama hicho, mjini Liwale na kueleza chanzo cha kushuka ukusanyaji korosho.

"Hali ya uchumi na uzalishaji wa chama chetu imeshuka, ikilinganishwa na uzalishaji msimu uliopita, kwani tani za korosho za msimu uliopita zina thamani ya Sh. bilioni 9, 271, 643, 280. 68," anasema.

**UZALISHAJI KUSHUKA**

Mpako anataja sababu kubwa ni hali ya hewa na upatikanaji wa pembejeo usiozingatia wakati, pia ukosefu wa utaalam wa matumizi sahihi ya dawa zinazotumika korosho.

"Chama chetu kitashirikiana kikamilifu na Idara ya Kilimo, ili kwa msimu ujao isije ikajitokeza tena na kuendelea kushuka kwa mapato na uzalishaji wa chama chetu," anasema.

Mwenyekiti huyo anawataka wanachama wenzake kuanzisha mashamba mapya, kutumia mbegu za kisasa na matumizi sahihi ya dawa, kuongeza uzalishaji wa chama chao.

"Sisi kama bodi, tutaendelea kusimamia kwa uadilifu na uaminifu, ili kupata huduma nzuri na za uhakika, kuwavutia wakulima ambao si wanachama, ili wauze korosho katika chama chetu," anasema.

**SOKO LA KOROSHO**

Pia, anataja changamoto nyingine waliokumbana nayo katika msimu uliopita, ni korosho kutouzwa kwa utaratibu uliozoeleka minadani.

Anataja chanzo kikubwa ni bei ya minada ya mwanzo kuwa ndogo na kusababisha wakulima kuikataa na kuifanya serikali kuingilia kati, kuepusha wakulima wasipate hasara.

"Kwa kuwa jambo hili ni la dharura, limelenga kumpa bei nzuri mkulima na malipo yalianza kwa awamu kwa kuanzia wakulima chini ya kilo 1,500 na hatimaye kulipwa wakulima wa zaidi ya kilo 1, 500," anasema.

Anasema serikali imewahakikishia wakulima kwamba kila mmoja atalipwa fedha zake na kuwataka wanachama kuendelea kuvuta subira, kwa vile serikali ilifanya maamuzi hayo kwa nia njema.

**MAPATO/ MATUMIZI**

Mpako anasema katika mwaka wa fedha 2018/19 kimefanikiwa kupata Sh. 600,000 za ushuru wa vibanda vya chama na Sh. 620,000 za viingilio vya wanachama, mradi wa kukodisha viti Sh.500,000.

"Zao la ufuta katika msimu uliopita tumefanikiwa kupata tani 69 , ambazo ushuru wake tumekusanya Sh. milioni 4.1, wakati pango la ghala kuu zilikusanywa tani 12,000 za korosho na tumelipwa na mpangaji wetu Sh.milioni 20 kati ya Sh. milioni 87 za pango," anasema. Mwenyekiti huyo anafafanua kuwa, mpangaji huyo ameahidi kumalizia kiasi kilichobakia cha Sh. milioni 67 mara tu baada ya kulipwa na serikali.

Aidha, anasema chama cha Umoja kimekusanya tani 2,813 zenye thamani ya Sh. bilioni 9, 271, 643, 280. 68, na kwamba tayari Sh. bilioni 6, 548, 143, 850.26 zimelipwa na serikali. "Hiyo ni kwa mujibu wa orodha ya majina tuliopewa kubandika kwenye mbao zetu za matangazo, kutoka kwa timu ya malipo Mtwara, ambayo ni Sh. 3,300 kwa kila kilo korosho daraja la kwanza na Sh. 2,640 daraja la pili," anasema.

Kwa mujibu wa Mpako, katika msimu wa mwaka 2017/2018 waliomba ridhaa ya wanachama kukopa Sh. milioni 500 kutoka Benki ya NMB, kwa ajili ya kujenga ghala kubwa na wamefanikiwa kupata mkopo huo na ujenzi umeshaanza.

"Ghala kuu ni mradi mama wa chama chetu. Pia, ni kitovu cha uchumi wa wilaya yetu na jamii inayotuzunguka na umetoa ajira na kuleta mzunguko wa fedha kwenye wilaya yetu," anasema.

Anasema ghala la sasa ni dogo lenye uwezo wa kukusanya tani 5,000 za korosho kwa wakati mmoja. Ndio maana wakafikia uamuzi wa kukopa pesa, ili kujenga lingine kubwa linaloweza kutunza tani 7,000.Mpako anasema, katika msimu wa mwaka 2017/2018, ghala ilipokea tani 17,000 na katika msimu uliopita lilipokea tani 12,000, ambazo ni nyingi kuliko uwezo wa ghala.

"Ombi langu kwenu, wanachama ni kwamba kila mmoja aendelee kukatwa Sh. 20 kwa kila kilo ya korosho ili kulipia mkopo wa Sh. milioni 500 tulizokopa kwa ajili ya ujenzi wa ghala jipya," anasema.

**MALENGO**

Mwenyekiti huyo anataja baadhi ya malengo ya chama hicho ni kuongeza wanachama zaidi. Anafafanua: "Unajua chama ni wanachama bila ya kuwa na wanachama siyo chama.Moja ya malengo yetu ni kuongeza idadi ya wanachama kadri inavyowezekana ili waendelee kuwa wengi." Anasema Umoja ina wanachama 1065, wakiwamo 21 waliojiunga na chama hivi karibuni na kutambulishwa kwenye mkutano mkuu wa chama mjini Liwale.

Historia ya chama, kilianzishwa mwaka 1988 kikiwa na wanachama 71, kati yao wanaume 60 na wanawake 11 na hadi sasa wameongezeka kufikia 1063.

Anasema wakati chama kinaanzishwa, idadi ya wanaume ilikuwa juu, lakini sasa imeshuka baada ya wanawake kutambua umuhimu wa ushirika na kujitokeza kwa wingi kujiunga nacho.

HABARI KIMATAIFA

# Marekani yaongeza tena ushuru kwa bidhaa za China

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI jana iliongeza tena kiwango cha ushuru kwa bidhaa za China, hatua ambayo China imesema italipiza kisasi.

Mzozo huo umeshika kasi kabla ya siku ya pili ya mazungumzo ya kibiashara kati ya viongozi wa nchi hizo kukutana.

Rais wa Marekani, Donald Trump, alipata ufafanuzi kutoka kwa wajumbe wake wa kibiashara baada ya kufanyika kwa mazungumzo ya kwanza kati yao na China.

Lakini, Rais Trump hakuchukua hatua yoyote kuhusu kutotangaza ushuru mpya, hivyo kuondoa matumaini kuwa huenda kukawa na ahueni katika dakika za mwisho wakati mazungumzo hayo yakiendelea.

Dakika chache baada ya Marekani kuongeza kodi kwa bidhaa za China za thamani ya Dola bilioni 200, kutoka asilimia 10 hadi 25, Wizara ya Biashara ya China ilisema kuwa imesikitishwa na uamuzi huo na kurudia ahadi yake ya kuchukua hatua mwafaka za kulipiza kisasi bila kufafanua.

Kufuatia mgogoro kati ya China na Marekani uliodumu kwa zaidi ya mwaka mmoja, maafisa kutoka nchi hizo mbili kubwa kiuchumi duniani walirejea kwenye meza ya mazungumzo juzi usiku, wakiongozwa na Naibu Waziri Mkuu wa China, Liu He mwakilishi wa Biashara wa Marekani, Robert Lighthizer na Waziri wa Fedha wa Marekani, Steven Mnuchin.

Liu He alisema kuwa anatarajia kuwa mazungumzo hayo yatakuwa ya wazi na ya tija kwa kila mmoja.

China inaamini kuwa kuongeza ushuru katika hali ya sasa sio suluhisho la tatizo hilo, bali kutaiumiza China, Marekani na ulimwengu mzima.

Alisema kulitatua tatizo hilo ni kupitia njia imara ili mwishowe kupatikane suluhisho pekee la ushirikiano.

Licha ya matumaini kutoka kwa maafisa wakati wa mazungumzo hayo yako kwenye mkondo wa kupata ufumbuzi, mivutano imezuka tena wiki hii baada ya RaisTrump kwa hasira kuituhumu China kwa kujaribu kulegeza ahadi zake.

Shirika la Fedha la Kimtaifa Duniani (IMF) limetoa wito wa kupatikana ufumbuzi wa haraka, likionya kuwa mapambano hayo ya kibiashara ni kitisho kwa ukuaji wa uchumi duniani.

Lilieleza kuwa ushuru ulioongezwa utaathiri vifaa vya kielektroniki vya China, mashine, vipuri vya magari na samani.

Lakini kutokana na mchakato wa utekelezwaji wa viwango hivyo vya ushuru, Ofisi ya Marekani ya Forodha na Ulinzi wa Mpakani ilieleza kuwa bidhaa ambazo tayari zinapelekwa katika bandari za Marekani kabla ya usiku wa manane zitalipa tu kiwango cha awali cha asilimia 10 ya ushuru.

Marekani inaishinikiza China kubadilisha sera zake kuhusu ulinzi wa hakimiliki za mali na kiwango kikubwa cha ruzuku kwa kampuni yanayomilikiwa na serikali, katika jaribio la kupunguza upungufu wa biashara.

Tangu mwaka jana, pande hizo mbili zimepandisha kodi za bidhaa za mwenzake za thamani ya zaidi ya Dola bilioni 360 katika biashara ya pande mbili na kuathiri bidhaa za kilimo za Marekani zinazouzwa China na kusababisha hasara kwa sekta za kutengeneza bidhaa za nchi zote mbili.

Taarifa ya Wizara ya Biashara ya China imesema wanatumai kuwa pande za Marekani na China zinaweza kukutana na kufanya kazi pamoja kuyatatua matatizo yaliyopo kupitia ushirikiano.

*DW*



# Trump ashtushwa mwanawe kuhojiwa

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amesema alishtushwa sana na hatua ya Kamati ya Upelelezi katika Baraza la Seneti, linaloongozwa na wabunge wa chama cha Republican kumtaka mwanawe mkubwa wa kiume, Donald Trump Junior, kufika katika kamati hiyo kuhojiwa.

Mtoto wa Trump ametakiwa kutoa maelezo zaidi kuhusiana na madai ya Russia kuingilia uchaguzi mkuu wa Marekani mwaka 2016.

Haijajulikana iwapo Trump Junior atafika mbele ya kamati hiyo kwa mahojiano licha ya kutakiwa kufanya hivyo na kamati inayoongozwa na wabunge wa Republican.

Uchunguzi wa mwendesha mashtaka maalum, Robert Mueller, ulimwondolea Rais Trump madai ya kampeni yake kushirikiana na Russia kumsaidia kushinda urais.

Mueller hata hivyo hakufikia maamuzi ya kumfungulia mashtaka Trump, katika madai ya kuwa alijaribu kuzuia sheria isifuate mkondo wake kwa kujaribu kuzuia uchunguzi wa Russia kufanyika.

Hata hivyo, Mwanasheria Mkuu William Barr, aliamua kwamba hakuna haja ya kumfungulia Trump mashtaka yoyote.

*VOA*



Ofisa wa Tume ya Uchaguzi ya Afrika Kusini, akimwaga kura tayari kwa kuhesabiwa, matokeo ya awali hadi jana yalionesha chama cha ANC kilikuwa kinaongoza. **PICHA: REUTERS**

# Waangalizi wasema uchaguzi Afrika Kusini ulikuwa huru na haki

**JOHANNESBURG, Afrika Kusini**

WAANGALIZI wa Kimataifa ambao wamekuwa wakifuatilia uchaguzi mkuu nchini Afrika Kusini, katika ripoti yao ya awali, wamesema uchaguzi huo ulikuwa huru, haki na wa amani.

Ripoti hii imekuja siku mbili baada ya raia wa nchi hiyo kupiga kura Mei 8 na matokeo ya awali yanaonesha kuwa chama tawala ANC kinaongoza na kinaelekea kupata ushindi.

Mwenyekiti wa waangalizi wa Umoja wa Afrika (AU), Rais wa zamani wa Tanzania, Jakaya Kikwete, alisema kuwa zoezi la upigaji kura liliendelea kwa amani na utulivu katika maeneo mengi ya nchi hiyo.

Aidha, aliongeza kuwa waangalizi wa Umoja wa Afrika wanasema Tume ya Uchaguzi ilijiandaa vema, kufanikisha uchaguzi huo, huku maafisa wa usalama wakitoa ushirikiano wa kuhakikisha kuwa usalama unakuwapo kipindi chote cha upigaji kura.

Hata hivyo, Kikwete alisema vijana wengi hawakuonekana wakipiga kura licha ya kuwa ndio wengi nchini humo, suala ambalo Umoja wa Afrika unataka wadau kuliangazia.

"Licha ya mambo mengine, kwenda vizuri, tuliona kuwa vijana wengi hawakujitokeza kupiga kura, hili ni suala ambalo linastahili kupewa ufumbuzi wa haraka," alisema Kikwete.

Waangalizi wa Mataifa ya Kusini mwa Afrika SADC pia walitoa ripoti yao ambayo pia imeeleza kuwa Uchaguzi huo ulikuwa huru na haki.

Wachambuzi wa siasa barani Afrika, wamekuwa wakisema miaka ya hivi karibuni, waangalizi wa Uchaguzi wamekuwa wakitumia mbinu za kidiplomasia, kutuliza joto la kisiasa katika mataifa mbalimbali ya Afrika.

Chama cha ANC ambacho kimekuwa madarakani tangu mwaka 1994, kinatarajiwa kushinda Uchaguzi huo kwa kati ya asilimia 55-59 huku kile cha EFF kikitarajiwa kumaliza katika nafasi ya tatu.

Tume ya Uchaguzi inatarajiwa kutangaza matokea ya mwisho, mwishoni mwa wiki hii.

*RFI*

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawatajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.
Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.

# Jumba Jekundu-1

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

GARI aina ya Subaru ilisimama kando ya barabara ya Kwa Mtogole maeneo ya Tandale jijini Dar es Salaam.

Hakuna yoyote aliyewatilia shaka watu wawili wenye miili mkubwa waliotoka ndani ya gari hilo na kufuata kinjia kidogo kilichoelekea kwenye daraja la mto Ng'ombe.

Ilikuwa ni kama wanasoma ramani kule walikokuwa wanaelekea kwa sababu hawakuwa wenyeji.

Safari yao iliishia kwenye kijumba kimoja kidogo ambacho kilikuwa kimejengwa peke yake.

Kwa hali ya kawaida kijumba kile kilitakiwa kuwa banda la uani na si nyumba iliyojengwa peke yake.


Ilionekana kama ilijengwa vyumba viwili na sebule, lakini haikupigwa 'lipu', matofali yake yakiwa ni makuukuu, huku juu kukiwa na mabati yaliyobadilika rangi kutoka ya asili na kuwa meusi kwa sababu ya kukaa kwa muda mrefu na kuwa na kutu.

Juu ya mabati hayo kulikuwa na matairi makuukuu ya gari, pamoja na baadhi ya matofali ambayo yote kazi yake ilikuwa moja tu, kukandamiza au kuzuia mabati hayo yasing'oke kwa upepo, kwani misumari iliyopigiliwa mabati hayo, ilikuwa imechoka, na baadhi ilikuwa imeshang'oka. Mabausa wale wawili walisimama nje ya nyumba hiyo walionekana kuongea, huku wakionekana kukubaliana kuwa walipokuwa wakipatafuta ni hapo.

Waliosogea kwa pamoja hadi kufika mlangoni. Ulikuwa ni mlango ambao nao haukueleweka ni rangi gani kutokana na rangi yake ya awali kuchujuka. Haukuwa na hadhi yoyote ya kuitwa mlango, zaidi ya kitu kilichowekwa hapo ili kuwahifadhi wanaoishi ndani wasionekane.

Kwa hali ya kawaida haukuwa na uwezo wa kumzuia hata kibaka kuupiga teke moja tu na kuingia ndani.

Mmoja aligonga mlango mara tatu. Ulifunguliwa nusu dakika baadaye. Aliyefungua ni kijana asiyezidi miaka 25. Alikuwa amevaa kaptura, pekupeku, mkononi akiwa na tonge la ugali. Kwanza alishangaa kuwaona aina ya wageni waliomtembelea. Si tu kwamba walikuwa ni wageni kwake, lakini pia walionekana ni watu mwenye miili mikubwa kwa sababu ya mazoezi, maarufu kama mabaunsa. Hakuwahi kuwa na rafiki wa aina ile.




Kwa mbali alihisi shari kwenye nyuso za wageni wake, lakini alijikaza, huku hofu ikianza kumuingia moyoni.

"Karibuni" Aliwakaribisha kwa sauti ambayo hata yeye mwenyewe alikuwa hana uhakika kama inatoka kwenye kinywa chake.

"Wewe ndiye Kadili?" Aliuliza baunsa mmoja ikiwa ni kama jibu ya ile karibu ya kijana yule ambayo haikujibiwa.

Kijana huyo alionyesha mshangao kiasi cha dakika moja, kana kwamba kuna kitu alikuwa akitaka kusema, lakini mwishowe akasema "Ndiye mimi."

"Unahitajika na Madame Pauline." Kuhitajika huko kulimshangaza sana Kadili. Hakuwahi kukutana na mtu wa aina hiyo.

"Ndiyo nani, mbona simjui?" Aliuliza.

"Sisi siyo jukumu letu kujua wewe unajua au humjui. Tumekuja kukuchukua wewe na kukupeleka kwa Madame Pauline ambaye ametutuma. Yeye anakufahamu kwa hivyo mtakwenda kutambua huko huko." Baunsa mwingine ambaye alikuwa hajaongea muda wote aliamua kuvunja ukimya.

Kwa kawaida yoyote yule anayekwenda kutaka kumchukua mtu ni lazima kwanza ajitambulishe hata kama ni askari, lakini hawa aliotaka kumchukua na kumpeleka kusikojulikana, Kadili aliona si sahihi kabisa. Ilitakiwa angalau mjumbe wa nyumba kumi ajue hili, lakini wageni wake hawakuonekana kutaka kufanya hilo na badala yake walikuwa waking'ang'ania kutaka kumchukua kama mzigo.

Alitaka kuongea hayo kwa mdomo, lakini hakuthubutu kwani wageni wake hawakuonekana kama ni watu wema hata kidogo na kutendo cha kutaka kuwafundisha jinsi gari taratibu, itakuwa ni kujitafutia balaa.

"Akina baba kwani imekuje?" Ilikuwa ni sauti mwanamke mnene mweusi aliyejifunga kilemba ambaye naye alitojitokeza kwenye kijumba hicho.

> **"Usiwe na wasiwasi mama, sisi tumetumwa na bosi wetu anaitwa Madame Pauline. Siyo mtu mbaya na hamuiti kwa nia mbaya na sisi wenyewe ndiye tutakaomrudisha."**

"Hapana mama. Hakuna kitu chochote kibaya, tunamhitaji huyu kijana Kadili tuondoke naye."

"Mnaenda naye wapi hivi hivi tu bila watu kujua mnampeleka wapi?"

"Usiwe na wasiwasi mama, sisi tumetumwa na bosi wetu anaitwa Madame Pauline. Siyo mtu mbaya na hamuiti kwa nia mbaya na sisi wenyewe ndiye tutakaomrudisha."

"Sasa mimi kama mama yake nitaamini vipi kama hachukuliwi kwa nia mbaya."

"Tunakuachia namba zetu, ukiona kimya basi piga au zipeleke polisi, lakini tunakuhakikisha kuwa atarudi tu."

Mama kwa sauti ya upole alimgeukia mwanae. "Kadili mwanangu, nenda, nenda nao tu. Mwenyezi Mungu atakulinda. Atakusaidia." Alipomaliza maneno hayo alizama ndani.

Kadili aliwatazama mabausa wale wawili kwa zamu.

"Basi naomba mnipe muda wa kujiandaa, nikavae kwanza."

"Sawa isichukue dakika tano." mmoja alijibu.

Alitoka nje akiwa amevaa fulana ya bluu iliyochoka. Suruali aina ya jeans iliyopauka na raba nyeusi.

"Twendeni." Aliwaambia.

Aliwekwa kwenye kiti cha mbele, akiwa pamoja na dereva, mabausa wale wakiwa amekaa kwenye siti ya nyuma.

Gari lilitaanza kutafuna lami kuelekea kule walikosema kuwa ni kwa Madame Pauline.

************************************

Akiwa kwenye likizo baada ya muhula wake wa pili kwenye Chuo cha Teknolojia, Kadili John alikwenda kwa rafiki yake Meze kwa ajili ya maongezi.

Katika maongezi yao walikumbushia enzi zao za kucheza disco, huku wakiwekeana ahadi kuwa mwishoni mwa wiki waende kujikumbushia enzi zao maeneo ya Sinza jijini Dar es Salaam.

"Mama Jumamosi nitaomba kwenda disco."

"Wapi?"

"Sinza"

"Sawa mwanangu, ila angalia wewe ni mwanafunzi na nakutegemea wewe. Usiende kufanya vitu ambavyo havielewiki, ukaja ukanitia hasara mimi mama yako. Dunia imeharibika hii."

"Najua mama, nakwenda na rafiki yangu Meze kwa hiyo hakuna wasiwasi na hilo unalosema nitalitekeleza."

Hayo yalikuwa ni maagano kati ya Kadili na mama yake akimuomba kwenda kuserebuka.

"Tayari mama amenikubalia kwa hiyo Jumamosi kama kawada Blue Star tunaingizana pale, uko fiti lakini kama zamani, nisije kukutoa 'know out'". Kadili alimkoga mwenzake.

"We uko chuoni huko sijui, lakini mimi huwa mara moja naenda disco ingawa mara moja moja, nikipata mtu wa kumuachia duka hapa." Alisema Meze ambaye anauza duka la mjombe wake.

**Itaendelea Jumamosi**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.
Baruapepe: ceo@kses.co.tz.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WUZHOU INVESTMENT**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI T.106 CQF AINA YA SANLG RANGI NYEKUNDU CHASSIS NAMBA LBRSPJB53D9026818 ENGINE NAMBA 13958199.

YEYOTE ATAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.

TAARIFA YA POLISI:
**RUS/RB/977/2019**.

115223402

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABDULKADIR JUMA MMBAGA**
OF TEMEKE SANDALI anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TRACTOR SWARAJ yenye namba za usajili T 978 CWZ Chassis namba WXCD45605194520. Engine NO.43.1025/STD05444.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**KLR/RB/1292/2017.**

215223202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Exaud Daniel Mambali**
anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili T197 CRH aina ya TOYOTA CARINA SI, Yenye chasis namba AT 2116067787, Engine namba 7AH957572.

Yeyote atayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**KMR/RB/2255/2019**

115222502

## KUPOTEA KWA KADI

**GEOFREY CHESCO KILANGI**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.186 BZQ** AINA YA MITSUBISHI FUSO CHASSIS NAMBA MK117F20262.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

**TAARIFA YA POLISI:**
**MB/RB/614/19**

215222102


NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA DODOMA**

**DODOMA**
**SHAURI LA MADAI NA. 18/2018**

**ALLY BAKARI MNDOLWA.......................MDAI**

**DHIDI YA**

**KUYELA ENTERPRISES LTD...............MDAIWA**

Kwa kuwa mdai alifungua shauri la nadai dhidi yako katika mahakama hii ambalo liliendealea na hatua ya kusikilizwaji wa upande mmoja baada yaw ewe mdai kushindwa kuhudhuria katika mahakama hii kwa kuleta mwakilishi anayeruhusiwa au wakili.

Hivyo basi mahakama hii inakupa taarifa kuwa shauri hili limepangwa katika hatua ya kusomwa hukumu ya upande mmoja tarehe 14/5/2019.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na cha ya mahakama hii leo tarehe 10/5/2019

HAKIMU WA MAHAKAMA YA WILAYA
DODOMA

115223002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO.
Usimamizi wa mirathi No; 95/2019
Ombi la AESHI MUSTAFA FADHILI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ABDALA AMIRIWatu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 16/05/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa
Tarehe 16/04/2019.

115222902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

**YAH: RUFAA NAMBA 19 LA 2018**

**ANASTAZIATHOMAS ............MDAI**
**DHIDI YA**
**KLEDO PAISON........MDAIWA**

**KWA: KLEDO PAISON – POPOTE ULIPO**
**KLEDO PAISON**, amefungua Rufaa mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Tanga dhidi yako. Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 29/5/2019 saa tatu kamili asubuhi (3:00). Hivyo basi,unatakiwa kufika katika Baraza hili bila kukosa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba ( W ) Tanga. Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande mmoja.

AMRI hii imetolewa na kutiwa saini Muhuri/Lakili wa Baraza hili leo tarehe 09/5/2019

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
TANGA

215222402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO Usimamizi wa mirathi No; 106/2019
Ombi la ALLY SAIDI SAKOLO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SAIDI ALLY SAKOLOWatu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 21/05/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa

Tarehe 10/05/2019.

115223002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: **MJINI MOROGORO** Usimamizi wa mirathi No; 103/2019

Ombi la RHODA G MWAKIBINGA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu OSWARD JOHN CHUMA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 06/06/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa

Tarehe 02/05/2019.

115111702


JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



### LIVERPOOL NA SPURS ZAMCHANGANYA MOURINHO

**LONDON, England**

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho amesema kwamba fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya itakayozikutanisha Liverpool na Tottenham tayari imeshamuweka njia panda, kwa sababu hajui ni timu ipi aishangilie.

Kauli ya Mourinho aliitoa wakati wa mahojiano kwenye beIN Sports, huku akisema ushindi wa Spurs umeibua ushindano mpya baina ya timu hizo mbili kutoka England zitakazokutana kwenye fainali hiyo.

Aliongeza kuwa mpambano huo utakuwa mkali kutokana na timu zinazokutana kwenye fainali zinatoka katika ligi moja.

Alisema licha ya soka kuwa burudani lakini ushindi ndio muhimu zaidi.

Aliweka bayana kwamba siku hiyo huenda akawa kwenye wakati mgumu kwa sababu anawakubali Pochettino na Jurgen Klopp mno na kusema kuwa anaamini wote wanastahili kutwaa taji hilo.

Hata hivyo, Mreno huyo alimsifu kocha Jurgen Klopp kutokana na falsafa yake ya kutokata tamaa.

Alisema jambo pekee la muhimu lililowavusha Liverpool ni kutokana na kikosi hicho kuwa na mawasailiano baina ya wachezaji wanapokuwa uwanjani.



# POGBA

## AWAGONGANISHA SOLSKJAER, WOODWARD

**MANCHESTER, England**

KOCHA Ole Gunnar, Solskjaer na bosi wake Ed Woodward, wametofautiana kuhusu hatima ya kiungo Paul Pogba katika kipindi hiki cha kuelekea usajili wa majira ya joto.

Solskjaer amepanga kupitisha panga kubwa pale Old Trafford mwishoni mwa msimu huu baada ya kikosi hicho kukosa nafasi ya kucheza mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao na kwamba apata sapoti yote kutoka kwa makamu mwenyekiti Woodward kuhusu usajili.

Lakini, shida imebaki kwenye jambo moja tu, Manchester United itafanya nini na mchezaji wao ghali Pogba, ambaye anataka kuyafikisha mwisho maisha yake kwenye kikosi hicho cha Old Trafford.

Pogba amebakiza miaka miwili kwenye mkataba wake na United ina kipengele cha kumwongezea mwaka mmoja zaidi, lakini staa huyo anataka kwenda Real Madrid huku akitamba kwamba miezi 12 iliyopita aligomewa kwenda Barcelona na bosi Woodward.

Taarifa za karibuni zinadai kuwa, Pogba sasa anataka kuondoka na aligoma kuzungumza na vyombo vya habari wakati timu hiyo ilipochapwa mabao 2-0 na Manchester City akihofia angezungumza kitu kingemfanya ajutie.

United imekuwa ikisisitiza kwamba mchezaji huyo hauzwi licha ya kutajwa kwa bei yake kuwa ni pauni milioni 140, ambayo Real Madrid wanaomba ipunguzwe.

Bosi Woodward hataki kumuuza Pogba, lakini kocha Ole ameshaamua kuijenga timu yake mpya kupitia kiungo, Scott McTominay msimu ujao. Shida ni kwamba Pogba ni mchezaji wa Adidas, ambao ndio wanaotengeneza jezi za wababe hao wa Old Trafford.

Ole hataki kubaki na mchezaji ambaye moyo wake haupo tayari kuichezea United, hivyo anataka kumuuza ili kupata pesa za kufanya usajili wa mastaa watakaokuwa tayari na siriazi kwenye kuitumikia timu hiyo.

## Madrid yajipanga kumng'oa Mbappe

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, anataka kumnasa Kylian Mbappe kwa vile anaamini 'dili' za Eden Hazard kutoka Chelsea na Paul Pogba kutoka Manchester United ni kama zimeshakamilika.

Madrid, ambayo pia inamfukuzia Neymar, imeandaa ofa itakayovunja rekodi ya dunia kwa ajili ya kutaka kumsajili mshambuliaji huyo wa PSG, Mbappe.

Kwa mujibu wa Gazeti la 'France Football', Madrid imeandaa ofa ambayo ni ngumu PSG kuikataa ya Euro 280 milioni ambayo itavunja rekodi ya pesa ambayo mabingwa hao wa Ufaransa walitoa (Euro milioni 222) mwaka 2017 kumnunua Neymar kutoka Barcelona.

Kocha Zidane, anataka kumnasa Mbappe kwa vile anaamini mchakato wa kumpata Hazard na Pogba unaweza kushindwa kukamilika katika kipindi cha majira ya joto kama walivyofikiria.

Hata hivyo, PSG haiko tayari kuwauza nyota wake kwa bei yoyote ile. Klabu hiyo inataka Mbappe awe sura ya klabu hiyo, lakini kumuuza kutaiondolea jinamizi la adhabu ya Financial Fair.



# Neymar nusuru azitwange na Draxler

**PARIS, Ufaransa**

NYOTA wa klabu ya Paris Sain Germain, Neymar anadaiwa kurushiana maneno makali na mchezaji mwenzake, Julian Draxler kwenye chumba cha kubadilishia nguo baada ya timu yake kupokea kichapo cha mabao 3-2 kutoka kwa Montpellier, Aprili 30 mwaka huu.

Neymar ambaye siku takribani 11 zilizopita aliingia matatani baada ya kuonekana akimpiga ngumi shabiki, anadaiwa kurushiana maneno makali na Draxler kwenye chumba cha kubadilishia nguo baada ya timu yake kupokea kichapo cha mabao 3-2 kutoka kwa Montpellier, Aprili 30.

Baada ya kichapo hicho, Draxler anadaiwa kutoa maneno ya ukali kwa wachezaji wenzake akiwatuhumu kufanya uzembe uliopelekea wapinzani wao kusawazisha mabao mawili na kupata la ushindi, kitendo ambacho kilimkera Neymar ambaye aliamua kujibizana na kiungo mshambuliaji huyo.

"Wewe ni nani hadi uniambie maneno kama hayo? Mtu mwenyewe unapiga pasi za kurudi nyuma tu!', Neymar aliongea kwa hasira kujibu Draxler jambo lililotaka kuibua mzozo baina yao ingawa ulitulizwa kabla haujapamba moto.

Matukio hayo ya utovu wa nidhamu wa mfululizo ambayo yamekuwa yakifanywa na Neymar, yameendelea kutokea katika kipindi ambacho wengi wanamkosoa Neymar kwa mchango duni anaoutoa ndani ya kikosi cha PSG licha ya yeye kuwa ndio mchezaji mwenye thamani kubwa kikosini.

Nyota huyo wa Kibrazil, analipwa kitita cha pauni 515,000 kwa wiki baada ya kukatwa kodi, lakini mafanikio pekee ambayo ameyapata ndani ya timu hiyo ni kutwaa taji la Ligi Kuu Ufaransa tu.






# BECKHAM
## MARUFUKU KUENDESHA GARI

**LONDON, England**

DAVID Beckham amepigwa marufuku kuendesha gari nchini England kwa muda wa miezi sita baada ya kupatikana na hatia ya kutumia simu wakati akiendesha.

Nahodha huyo wa zamani wa England alikiri makosa hayo na kupatiwa adhabu hiyo ya kutoendesha gari.

Mahakama iliarifiwa kwamba alipigwa picha na raia akiwa ameshikilia simu wakati akiendesha gari lake aina ya Bentley 'taratibu' katika foleni.

Beckham, mwenye umri wa miaka 44, ametozwa faini ya pauni 750, ameagizwa alipe pauni 100 kwa ajili ya gharama ya kesi na malipo ya ziada ya pauni 75 katika siku saba zijazo.

Jaji katika mahakama hiyo amemwambia hata kama kasi ya gari ilikuwa taratibu kwenye foleni 'hakuna kisingizio' chini ya sheria.

Mwendesha mashtaka alisema: "Badala ya kutazama mbele na kuangalia barabara alionekana akitazama mapajani mwake."

Wakili wa Beckham, Gerrard Tyrrell amesema mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United hakumbuki siku hiyo au tukio hilo.

Aliongeza: "Hakuna utetezi wa kilichotokea, lakini mtazamo wake ni kwamba hakumbuki."

Tyrrell ameiambia mahakama kwamba Beckham hufurahia kuendesha gari.

"Huwapeleka watoto shuleni kila siku na mara nyingine hurudi kuwachukua anapoweza, lakini kwa sasa hana budi kulikubali," amesema.

Ni kinyume cha sheria nchini Uingereza kushika simu wakati unaendesha gari, kwani mtu anaweza kuadhibiwa kwa kupunguziwa pointi kwenye leseni na kutozwa faini ya pauni 200.

# Klabu zapinga mageuzi Ligi ya mabingwa Ulaya

**MADRID, Hispania**

KLABU za soka barani Ulaya zimelitaka shirikisho la vyama vya soka Ulaya, (Uefa), kuzishirikisha vizuri katika mipango yake ya kubadili mfumo wa Ligi ya Mabingwa, ambayo inaweza kuihakikisha kwa timu vigogo kucheza kwenye mashindano hayo mara kwa mara.

Rais wa Ligi Kuu Hispania (La Liga), Javier Tebas, ambaye alikuwa mmoja wa wawakilishi zaidi ya wajumbe 300 waliohudhuria mkutano jijini Madrid, pia alisema "uwezekano wa kuchukua hatua za kisheria umeangaliwa" iwapo UEFA itang'ang'ania kuendelea na mageuzi hayo yasiyotakiwa.

Tebas alisema ana uhakika "kesi yoyote itakayofunguliwa mahakamani itakuwa na mafanikio".

Mkutano huo ulikutanisha pamoja klabu 244 kutoka nchi 38, ukiwa na lengo la kutengeneza mazingira ya maelewano kabla ya mkutano wa leo Jumatano kati ya viongozi wa Ligi za Ulaya na Kamati ya Utendaji ya UEFA unaofanyika jijini Nyon, Uswisi.

Mabadiliko katika michuano ya klabu ya Ulaya yamekuwa ni suala lenye utata baada ya Andrea Agnelli, Rais wa Chama cha Klabu za Ulaya (ECA), kuwasilisha mapendekezo kwa ajili ya mfumo wa ligi moja ya Ulaya" ambao kwa kiasi kikubwa utapunguza idadi ya timu zinazofuzu kutoka ligi za nchi wanachama.

Lakini Tebas alisema katika mkutano na waandishi wa habari kuwa "haiwezekani kufanya mabadiliko bila ya makubaliano na ligi za nchi. Sijui inawezekana vipi kubadili kitu chochote bila ya makubaliano na mashindano ya taifa ya nchi."

Mwenyekiti wa Umoja wa Ligi za Ulaya, Lars-Christer Olsson aliongeza kusema: "Ligi za Ulaya na wanachama wetu wote wamesema hatuna budi kushirikishwa vizuri katika kufanya maamuzi kuhusu hali ya baadaye ya mashindano ya Ulaya.

"Mchakato hauna budi kubadilika kutoka katika (utaratibu wa ) kututaarifu tu kwenda katika (utaratibu wa) kujadiliana nasi."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# NI ARSENAL VS CHELSEA FAINALI LIGI YA EUROPA

●●● Ni fainali nyingine Ulaya ambayo inakutanisha klabu zote kutoka England...

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Arsenal Pierre-Emerick Aubameyang aliifungia timu yake mabao matatu 'hat-trick' na kuisaidia kutinga hatua ya fainali ya Ligi ya Europa ambapo watakutana na Chelsea wakati wakiifunga Valencia jumla ya mabao 7-3.

Washikabunduki hao sasa wanasubiri ushindi wa fainali hiyo ili kujikatia tiketi ya kushiriki katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku kocha Unai Emery akiweka historia ya kushinda taji hilo mara nne.

Wakati huo huo Eden Hazard alifunga penalti ya mwisho na ya ushindi akiisaidia Chelsea kuilaza Eintracht Franfurt 4-3 kwa mikwaju ya penalti na hivyo basi kukutanisha timu mbili za Uingereza katika fainali hiyo.

Hazard ambaye huenda angecheza mechi yake ya mwisho kwenye Uwanja wa Stamford Bridge, alifunga penalti ya mwisho baada ya kipa Kepa Arrizabalaga kuokoa mikwaju miwili ya penalti kutoka kwa Hinteregger na Goncalo Paciencia.

Hii ni mara ya kwanza kwa timu nne za Uingereza kuingia katika fainali za makombe mawili ya Ulaya.

Huku ikiwa na matokeo ya 1-1 baada ya mkondo wa kwanza, Chelsea ilichukua uongozi katika kipindi cha pili baada ya Reuben Loftus Cheek kucheka na wavu dakika ya 28 lakini usiku huo ulikuwa mrefu sana kwa Chelsea.

Frankfurt ilisawazisha dakika nne tu baada ya kipindi cha pili wakati Luka Jovic alipomfunga Arrizabalaga kufuatia pasi nzuri kutoka kwa Mijat Gacinovic.

Bao la Jovic iliiadhibu Chelsea baada ya kuanza vibaya katika kipindi cha pili huku the Blues wakizidi kushindwa kujimudu. Wakiwa nyuma 3-1 kutoka katika mkondo wa kwanza, mjini London, bao la Kevin Gameiro lilikuwa limewapatia wanyeji hao mwamko mpya.

Hata hivyo, goli la Aubameyang kutoka umbali wa mita 20 lilisawazisha kabla ya Alexandre Lacazette kuiweka kifua mbele Arsenal baada ya kufunga goli la kiwango cha juu.

Gameiro ambaye ameshinda taji hilo mara nne na klabu ya Sevilla na Atletico Madrid, alifunga bao la pili kabla ya Aubemayang kufunga goli la tatu.

Mshambuliaji huyo wa Gabon aliteleza na pasi ya Ainsley Maitland-Niles hadi wavuni kabla ya kufunga bao la nne na kukamilisha hat-trick yake huku akiisaidia Arsenal kuilaza Valencia 4-2 nyumbani.

Hatua hiyo, inamaanisha kwamba Arsenal ambayo ilicheza mechi yake ya kwanza dhidi ya klabu ya FK Qarabag nchini Azerbaijan itarudi katika taifa hilo katika mechi ya fainali dhidi ya kikosi cha Maurizio Sarri siku ya Jumatano Mei 29 mwaka huu.

Itakuwa fainali ya kwanza inayoshirikisha mataifa mawili ya Uingereza tangu Tottenham ilaze Wolves katika mikondo miwili mwaka 1972, wakati mashindano hayo yalipokuwa yakiitwa Uefa Cup na itakua mara ya kwanza kwamba timu zote nne zilizofuzu katika mashindano mawili ya Europa yanatoka katika taifa moja.

## KWA UFUPI

### HAZARD AKWAA KISIKI

KIUNGO wa Chelsea, Eden Hazard (28) anataka kukamilisha mchakato wa kuhamia Real Madrid mapema iwezekanavyo, lakini klabu yake maarufu The Blues imesema haitakuwa tayari kumuuza Mbelgiji huyo kwa dau la chini ya pauni milioni 100. ***(ESPN)***

### COUTINHO KUIKAMUA UTD

MANCHESTER United italazimika kulipa kiasi cha pauni Euro milioni 100 kama wanataka kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Philippe Coutinho. Mbazil huyo mwenye umri wa miaka 26, ni mmoja wa nyota 10 wanaotarajiwa kuondoka Nou Camp katika kipindi cha majira ya joto. ***(AS - in Spanish)***

### GUARDIOLA ABADILI MAWAZO

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola ameamua kusitisha uamuzi wake wa kumwania mshambuliaji wa Sporting Lisbon Mreno, Bruno Fernandes ambaye ana umri wa miaka 24. ***(The Sun)***

### FERNANDES ATAKIWA UTD

KATIKA kutaka kuimarisha kikosi chake, Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ameweka wazi anamhitaji nyota, Bruno Fernandes (24) kutoka Sporting Lisbon ya Ureno. ***(ESPN)***

### NEYMAR KUONDOKA PSG

STRAIKA wa Timu ya Taifa ya Brazil, Neymar, amebadilisha mawazo kuhusu hatima yake ndani ya kikosi cha Paris St-Germain na kuweka wazi kwamba sasa anataka kuondoka kwenye timu hiyo. ***(Le10Sport)***

### PSG YAIZIDI ARSENAL

MATUMAINI ya Arsenal kumsajili winga wa Lille, Nicolas Pepe yamepotea kufuatia Paris St-Germain kuongoza katika mbio za kumnasa nyota huyo mwenye umri wa miaka 23 na raia wa Ivory Coast. ***(Sun)***

### TOBY KUREJEA AJAX

BEKI wa Tottenham, Toby Alderweireld amesema kuwa uamuzi wa kurejea Ajax uko katika mawazo yake kwa asilimia "100% ". Mbelgiji huyo mwenye umri wa miaka 30, alikuwa mjini Amsterdam kati ya mwaka 2008 na 2013, akiitumikia klabu hiyo. ***(Voetbal International via Sky Sports)***

### MORATA KUREJEA ATLETICO

ATLETICO Madrid italazimika kuilipa Chelsea kiasi cha Euro milioni 18 ili kumrejesha katika kikosi chake straika Mhispania Alvaro Morata ambaye mkataba wake wa mkopo klabuni hapo umebakiza msimu mmoja. ***(AS - in Spanish)***

### BARCA KUTEMA NYOTA 10

BARCELONA inatarajia kuwaachia wachezaji wake 10 kwenda kujiunga na timu nyingine katika kipindi cha majira ya joto, kati ya wachezaji hao yupo mshambuliaji, Philippe Coutinho, beki Samuel Umtiti na kiungo, Ivan Rakitic. ***(AS)***

### ROSE AJIPANGA VEMA

BEKI wa kushoto wa Tottenham na England, Danny Rose, amesema kuwa anajiandaa kumaliza vema msimu huu kama mwezi ujao katika mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya itakuwa ndio mchezo wake wa mwisho kwa Spurs. Rose (28), aliongeza kuwa anaona kuna dalili za "yeye kuuzwa". ***(Mirror)***

### AJAX: LIGT NJIA MOJA

NAHODHA na beki wa Ajax, Matthijs de Ligt (19), huenda akahamia England au Hispania katika kipindi cha majira ya joto, kauli hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mtendaji, Edwin van der Sar. Mholanzi huyo anahusishwa na tetesi za kujiunga na Barcelona. ***(Sky Sports)***

### MITROVIC SOKONI

MABOSI wa Southampton wanatarajia kutoa kiasi cha pauni milioni 30 ili kumsajili straika wa Fulham na Timu ya Taifa ya Serbia, Aleksandar Mitrovic (24). ***(Express)***

### SHEFFIELD KUSAJILI MKONGO

TIMU iliyopanda daraja na kucheza Ligi Kuu England msimu ujao, Sheffield United imeonyesha nia ya kumsajili straika wa Middlesbrough ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Britt Assombalonga (26). ***(Northern Echo)***

HABARI MICHEZO

# SIRI YA USHINDI WA SIMBA LIGI KUU HII

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI Emmanuel Okwi na Meddie Kagere wa Simba, wamesema kuwa siri kubwa inayowapata ushindi katika timu yao ni umoja, ushirikiano na hamasa baina yao na wachezaji wengine wa klabu hiyo.

Nyota hao waliliambia gazeti hili kwa nyakati tofauti baada ya kumalizika kwa mchezo dhidi ya Coastal Union kutoka jijini Tanga, ambao kila mmoja alifunga 'hat-trick'katika ushindi wa mabao 8-1.

"Nawapongeza wachezaji wenzangu kwa sababu tumecheza mechi nyingi sana kwa muda mfupi na tumekuwa na muda mfupi wa kupumzika, lakini tunamshukuru Mungu tumekuwa tukipata matokeo mazuri. Lakini pia nashukuru kwa kuisaidia timu yangu kupata ushindi," alisema Okwi.

Kuhusu kurejea tena kwenye kiwango chake kwa siku za karibuni, huku akifunga magoli karibuni kila mechi Okwi alisema kuwa alisaidiwa zaidi na wachezaji wenzake.

"Siri ni kutokata tamaa na pia kuwa na ushirikiano mzuri na wachezaji wenzangu kwa sababu unapokuwa haupo sawa, halafu wachezaji wenzako wanakupa ushauri, wanakuhamasisha, wanakusaidia uwanjani, tunasaidiana, tunapambana na hakuna kukata tamaa." Okwi aliongeza.

Kwa upande wa Kagere, straika wa zamani wa Gor Mahia ya Kenya, alisema wamekuwa wakipata ushindi mfululizo kutokana na kucheza kwa ushirikiano, kwani bila hivyo ingekuwa kazi bure.

"Wachezaji tumekuwa tukipendana na hii hata mimi imenisaidia kufikisha magoli 10, kupata 'hat-trick' na timu kupata ushindi." alisema.

Kuhusu ufungaji bora alisema kuwa atajitahidi kufunga magoli na kuangalia mwisho wa Ligi Kuu hali itakuwaje.

Hadi kufikia jana, tayari jumla ya 'hat-trick' tano zimeshafungwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, mbili zikifungwa na Okwi, Kagere, Alex Kitenge na Salum Aiyee.

Kabla ya mechi ya jana dhidi ya Kagera Sugar, Simba imeshinda mechi 26, sare tatu na kupoteza mechi mbili katika ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na inayotarajiwa kumalizika ifikapo Mei 28 mwaka huu.




Golikipa wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga akiruka na kupangua penalti iliyopigwa na nyota wa Eintracht Frankfurt, Goncalo Paciencia, katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Europa iliyochezwa juzi. Chelsea ilisonga mbele kwa penalti 4-3. **PICHA: MTANDAO**

# Viingilio kuiona Sevilla hadharani

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limetangaza kiingilio cha chini katika mchezo wa kimataifa wa kirafiki kati ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba dhidi ya Sevilla FC kutoka nchini Hispania kuwa ni Sh. 5,000.

Mechi hiyo ya kirafiki inatarajiwa kuchezwa Mei 23 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kuanzia majira ya saa 1:00 Usiku.

Mkurugenzi wa Fedha na Utawala wa TFF, Cornel Barnaba, alisema kuwa lengo la kuweka kiingilio hicho ni kutoa fursa kwa mashabiki wengi kuhudhuria katika mchezo huo na kutaja viingilio vingine vitakuwa ni Sh. 15,000 na cha juu ni Sh. 100,000.

"Kutakuwa na kiingilio cha Platinum ambacho gharama yake ni sh. 100,000, na hapa walengwa watapewa usafiri wa kwenda uwanjani kutoka hoteli ya Serena na kurudishwa, tiketi za mechi pamoja na chakula na vinywaji wawapo uwanjani," alisema mkurugenzi huyo.

Aliwataka pia mashabiki wa soka kukata tiketi mapema ili kuepuka usumbufu.

Naye Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa Kampuni ya SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas alisema kuwa wamemua kuweka mechi jioni ili kutoa fursa kwa kila Mtanzania kuja kushuhudia.

"Tunajua mechi itachezwa wakati wa Mfungo wa Ramadhan hivyo tumeamua kuruhusu wajasiriamali wanaouza futari kuja kuuzia uwanjani ili watu wapate kufuturu kabla ya kuingia kwenye mechi," alisema Tarimba.

Sevilla watatua nchini siku mbili kabla ya mchezo huo na pia wanatarajiwa kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii huku pia wakishiriki katika kliniki za soka na kutoa mafunzo kwa viongozi wa soka wa hapa nyumbani.

# Baobab Queens walilia udhamini

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

UONGOZI wa Baobab Queens unawaomba wadau mbalimbali wa michezo jijini hapa kujitokeza kuisaidia timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Kauli hiyo imetolewa baada ya Baobab Queens kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Alliance Girls kutoka Mwanza na kufikisha pointi 19 katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini hapa.

Mabao yote ya wenyeji yalifungwa na Neema Paul huku lile la kufutia machozi la Alliance likipachikwa wavuni na Rachel Kamanda.

Akizungumza na gazeti hili, Mwenyekiti wa Baobab Queens, Innocensia James, alisema kuwa licha ya wachezaji wake kupambana kusaka matokeo mazuri, timu hiyo inaendeshwa katika mazingira magumu sana.

Kiongozi huyo alisema kuwa umefika wadau mbalimbali hasa walioko Dodoma wakajitokeza kuwasaidia na kuwadhamini ili waweze kufanya vizuri katika ligi hiyo na kupeperusha vema bendera ya jiji la Dodoma.

Aliongeza kuwa Dodoma ni makao makuu ya nchi na ni vema wakazi wa jiji hilo wanajivunia kuwa na timu inayoshiriki Ligi Kuu kama zilivyo klabu nyingine ambazo zinachuana katika ligi za madaraja mengine.

**"Baobao ni timu pekee inayocheza Ligi Kuu katika mkoa wa Dodoma, hivyo ni muhimu kuiwezesha timu hiyo ili iweze kubaki na kuwakilisha makao makuu, tunaendelea kuwashukuru wote ambao wamekuwa wakitusaidia kwa kutupa michango ya aina mbalimbali, tunawaahidi hatutawaangusha," aliongeza kiongozi huyo.**

Aliwataka wakazi wa jiji hilo kuendelea kujivunia timu yao hiyo inayoshiriki ligi ya juu kwa upande wa soka la wanawake baada ya kushindwa tena kupandisha timu kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu ujao.

# Michezo

Jumamosi Mei 11, 2019

Nipashe



Ni Arsenal vs Chelsea fainali Ligi ya Europa

HABARI UK 30




Kiungo wa Arsenal, Mesut Ozil (kulia), akiondoka na mpira baada ya kumpiga chenga nyota wa Valencia, Francis Coquelin katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Europa iliyochezwa juzi usiku. Arsenal ilishinda mabao 4-2. **PICHA: MTANDAO.**

# SIMBA, YANGA HAWACHEKANI

## Zakubali vichapo kutoka kwa Kagera Sugar na Biashara United...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI Kagera Sugar imeendeleza ubabe kwa kuifunga Simba bao 1-0 katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jana, Yanga pia imeangukia "pua" huko Musoma kwa kufungwa idadi hiyo ya goli na wenyeji Biashara United, katika mchezo mwingine wa ligi hiyo.

Kwa matokeo hayo, Kagera Sugar iliyocheza mechi 35, sasa imefikisha pointi 43 ikiwa ndiyo timu pekee iliyovuna pointi sita kutoka kwa Simba msimu huu baada ya kupata ushindi wa mabao 2-1 katika mchezo wao uliopita ambao ulichezwa Aprili 20 mwaka huu kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

Hata hivyo, mabingwa hao watetezi wanaendelea kukaa juu katika msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 81 huku wa wamecheza mechi 31 wakifuatiwa na Yanga yenye pointi 80, lakini imeshuka uwanjani mara 35.

Bao hilo pekee la Kagera Sugar lilifungwa na beki wa Simba, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr' katika harakati za kuokoa hatari langoni mwake huku wakishindwa kuwasiliana vema na kipa wake, Aishi Manula dakika ya 41. Simba ilikaribia kupata bado la kusawazisha lakini mshambuliaji wake chipukizi, Rashid Juma hakuonekana kuwa makini kila alipokuwa jirani na lango la wapinzani wao huku Meddie Kagera na Mganda Emmanuel Okwi wakionekana kukosa bahati katika mchezo wa leo.

Dakika ya 67 Simba walipoteza nafasi nyingine ya kufunga katika mchezo huo baada ya kipa wa Kagera Sugar, Said Kipao kudaka kirahisi shuti dhaifu lililopigwa na Zana Coulibaly ambaye alimalizia pasi fupi iliopigwa na Clatous Chama huku Okwi akiwa jirani anasubiri kumalizika shambulizi hilo kama angetengewa mpira huo.

Tariq Seif ndiye aliyewanyanyua mashabiki wa Biashara United kwa kufunga bao hilo pekee la dakika ya tisa na kuifanya timu yake ifikishe pointi 40 na kuanza kujinyanyua taratibu kwenye janga la kushuka daraja.

Kiungo Thabani Kamusoko, alipiga krosi safi lakini mshambuliaji, Heritier Makambo, alichelewa kuunganisha na kuinyima timu yake ya Yanga nafasi ya kupata bao la kusawazisha dakika ya 50 kwa kuruhusu mpira kutoka nje huku kipa wa Biashara United, Nurdin Balora, akidaka kiufundi shuti la Makambo aliyekuwa jirani na lango lake na kuwanyima Yanga nafasi nyingine ya kupata bao dakika ya 65.

Ushindi huo unaifanya Biashara United iliyocheza mechi 34 na inayofundishwa na beki wa zamani wa Simba kufikisha pointi 40.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea tena leo kwa African Lyon kuwakaribisha Ndanda FC wakati kesho Lipuli watacheza na Mbeya City, Coastal Union watavaana na Mtibwa Sugar wakati Mwadui itachuana na Mbao FC na Allaince itawafuata Biashara United.

Simba yenyewe itashuka tena uwanjani Jumatatu kucheza dhidi ya Azam FC na siku inayofuata Yanga watawakaribisha Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

## Lipuli mawazo yote kwa Azam

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kujihakikishia kutoshuka daraja msimu huu, timu ya Lipuli sasa imewekeza nguvu na mawazo yake ya kuhakikisha inapata ushindi katika mchezo wa fainali ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Azam FC utakaochezwa Juni Mosi kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi.

Lipuli FC imetinga fainali ya michuano hiyo baada ya kuwafunga Yanga mabao 2-0 wakati Azam FC wenyewe waliwafunga KMC goli 1-0.

Bingwa wa michuano hiyo ataiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika hapo mwakani wakati klabu itakayochukua taji la Ligi Kuu itashiriki Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kocha wa Lipuli, Selemani Matola, alisema kuwa mechi hiyo ya fainali ya FA kwao ni muhimu kuliko mechi nyingine zilizosalia msimu huu kwa sababu wanahitaji kushiriki michuano ya kimataifa na kuweka historia kwenye timu hiyo.

Matola alisema kuwa wanawaomba wadau wa timu hiyo waendelee kuwaunga mkono ili malengo yao yaweze kutimia kama ambavyo waliamini wakati wanaanza msimu huu.

"Wakati tunaanza msimu wote tulikuwa katika nafasi sawa ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara, lakini siku zilivyokwenda, mbio zilipungua na wachache walibakia juu, sisi tunaona tuwekeze huku, tunamshukuru Mungu tumeingia fainali, tunajipanga kupata ushindi katika mchezo huo na hatimaye ndoto zetu kuwa kweli," alisema Matola.

Nahodha na kiungo huyo wa zamani wa Simba aliongeza kuwa amewaambia wachezaji wake kuongeza bidii kwa sababu wakifanikiwa kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, watatangaza vipaji vyao kwa mawakala wa ndani na nje ya nchi.

Kabla ya kuifunga Yanga katika mashindano hayo ya Kombe la FA, Lipuli ilipata kichapo cha mabao 3-0 na Biashara United na juzi ikakubali kufungwa magoli 2-0 na Ruvu Shooting katika mechi za Ligi Kuu Bara.

Mtibwa Sugar ya Manungu, Turiani mkoani Morogoro ndiyo ilikuwa inashikilia taji la mashindano hayo, lakini ilitolewa mapema na kulifanya kombe hilo kuwa huru.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >